

KUSHAWISHIKA KISHA KUHUSIKA



Asante sana, ndugu.

Ketini. Hakika ninahesabu haya kwamba ni majaliwa makuu, ya kuwa hapa usiku wa leo pamoja na Ndugu Groomer, na kwa kanisa lake, na kulisalimia kundi linalosafiri hapa Tempe, Arizona. Ninaamini huu. . .

² Je! huu ndio mji Wamormoni walioujenga hapa, ndio huu? [Ndugu wanasema, “La. Mesa.”—Mh.] Mesa. Ninajua ni mmoja wa hii miji midogo. Miaka mingi iliyopita, wakati nilipokuwa mvulana tu, katika kuwekwa wakfu kwa lile Hekalu la Mormoni. Sikukumbuka kama ilikuwa ni Tempe ama . . . Mesa ndiko ndugu walisema.

³ Nami daima ninachelewa, siwahi kamwe. Unajua, wananiambia nilikuwa kidogo tu zaidi ya wakati wa kawaida, kuwa humu duniani. Nilimfanya mke wangu kungojea muda mrefu, wakati tulipofunga ndoa. Laiti ningalichelewa tu kwenye mazishi yangu sasa; hilo, hilo ndilo jambo linalofuata. Huo ndio wakati ninaotaka kuchelewa, kuchelewa sana. Lakini watu wamekuwa wema kuningojea.

⁴ Niliingia kwenye dhoruba ya theluji na nikazuiliwa kwa siku kadhaa, kabla sijafika hapa, nami nimechelewa kwa siku mbili kwenye mkutano hapa pamoja na Ndugu Groomer. Nilipaswa kuwa hapa Jumanne iliyopita usiku. Lakini tumefanya matayarisho kusudi tupate kuyafikia yote, na, ama vyovyote walivyoandaa mambo. Huenda nikakosea kwenye jambo hili. Lakini wameandaa mambo, kwa hiyo nitayafikia, hata hivyo.

⁵ Jana usiku tulikuwa na mkutano mzuri sana, huko kwenye lile-lile kanisa lingine, nje, na Ndugu Hatton, ninaamini, naam, Ndugu Hatton, Mkristo muungwana mzuri sana. Nilikutana naye jana, na nikaketi kwenye chumba cha kusomea muda mfupi pamoja naye, nasi tulikuwa na wakati wa ushirika, tukaomba pamoja. Tulikuwa na ibada nzuri sana kule, jana usiku, bali tulikaa zaidi kidogo, nikawachelewesha watu. Hiyo kwa namna fulani ni tabia yangu. Lakini usiku wa leo sitafanya hivyo. La. Si—sikusudii kuhubiri kwa zaidi ya saa nne. Kamwe si—sitarajii kufanya hivyo. Kwa hiyo, unaona, hiyo karibu ni sawa, maskanini ama mahali fulani.

⁶ Ninaona baadhi ya marafiki zangu kutoka karibu na Jeffersonville, ama wanaotutembelea. Tuna watu walioketi hapa mbele zetu, usiku wa leo, ninaona, wanaoendesha magari kote kutoka Macon, Georgia, kila Jumapili. Ili kunini. . . Hiyo ni kama mia saba, elfu moja mia nne. . . Hiyo ni kama maili elfu moja mia tano, kwenda na kurudi, kuja kanisani Jumapili. Nao

hawafanyi jambo hilo wakati mmoja tu. Kila siku mwakani ambapo tuna ibada maskanini, wanaendesha magari kutoka huko mbali sana Macon, Georgia.

⁷ Ninawaona Ndugu na Dada Dauch hapa kutoka Ohio. Ndugu Dauch ana umri mkubwa mno, lakini ni yeye tu pamoja na mke wake, na Bwana amekuwa mwema kwao. Nao wana—wanaendesha gari kila Jumapili, hawa mke na mume wenye umri mkubwa, kutoka huko juu Ohio, wanashuka kutoka, kupitia kwenye barabara zenye barafu. Naye, mwanamke, aliendesha gari umbali wote kutoka Ohio, hadi hapa, apate kuwa kwenye mkutano huu.

⁸ Na hawa hapa watu, kutoka Macon na mahali mbalimbali, ambao wamekusanyika hapa kwa ajili ya ibada. Tunafurahi kuwa na marafiki kama hao. Tunafuraha sana kushiriki majaliwa yetu pamoja, ushirika wetu pamoja, kwa kuwa kweli tunakiri ya kwamba sisi ni wasafiri na wageni. Haya si makazi yetu.

⁹ Ninaamini, nimeangalia tu huku na kumwona ndugu kutoka mbali huko Iowa, hapa chini, kama hiyo ni kweli. Sivyo, ndugu? Huku, mkwe wa Ndugu Norman kutoka Iowa?

¹⁰ Sisi ni kama Ibrahimu. Sisi . . . tumeuacha ulimwengu. Nasi tunautafuta Mji ambao Mwenye Kuujenga na Kuubuni ni Mungu. Tunaamini ya kwamba, siku moja, siku yenye utukufu, tutauona Mji huo. Shauku yote ya moyo wangu ni kuuona Mji huo wenye utukufu.

¹¹ Sasa, tunamtumaini Mungu, kutubariki usiku wa leo, na kutupa Uwepo Wake.

¹² Nami nilikuwa tu nikisema jambo hilo kwa ajili ya badiliko dogo, mazingira, kwa ajili ya tabasamu kidogo, wakati niliposema, “Kuhubiri masaa manne.” Sasa, nina hatia ya kufanya hivyo, unaona, nao watu wana hatia ya kuketi na kusikiliza kwa muda mrefu hivyo. Lakini hilo—hilo ni gumu kidogo, kuwaadhibu namna hiyo.

¹³ Hili ni kanisa dogo lililojengwa vizuri. Karibu ninaweza kumwona kila mtu. Ungekuwa ni wakati mzuri, mahali hapa, kwa ajili ya ibada halisi ya uponyaji, kama tungekuwa na moja wakati fulani, kuifanya.

¹⁴ Ninaona, huko nyuma kabisa, ninamwona Dada Evans huko nyuma. Simwoni Ndugu Evans. Wao pia wametoka huko Macon, Georgia, huko chini kabisa kwenye nchi ya joto. Walizungumza nasi hivi majuzi, na wakasema walikuwa wakijilipizia kisasi nasi Wamarekani kule. Walikuwa na inchi tisa za theluji. Kwa hiyo, wao, kitu fulani cha kujivunia, kuwa na theluji hiyo yote. Je! ulikuwa na safari njema huko? Hilo, vema, hilo ni sawa kabisa, Ndugu Evans.

¹⁵ Ushuhuda mdogo tu kwa ajili ya Ndugu Evans kule nyuma, ambao ningependa kutoa, kama ni sawa kwako, Ndugu Evans. Kama ni. . .

¹⁶ Jinsi nilivyopata kumjua Ndugu Evans, ilikuwa kule—kule Met, huko Philadelphia. Ndugu Theo Jones, wengi wenu mmemsikia, yeye ni ndugu wa Full Gospel, mhubiri mzuri sana. Nasi tulikutana, naye akaniuliza kama ningekuja huko Met pamoja naye kwa ajili ya ibada za siku chache usiku, nami nikakubali kufanya hivyo tulipokuwa tukija kutoka mahali fulani. Nao Ndugu Leo Mercier na Ndugu Gene Goad walikuwa wamekwisha fahamiana na Ndugu Evans kwa namna fulani, nao wakasema, “Kuna mtu anayetaka kukutana nawe kwenye moja ya mahojiano ya faraghani,” kasema, “kutoka huko chini Georgia.”

Nami nikasema, “Vema.” Na mke wangu na mvulana mdogo. . .

¹⁷ Joseph mdogo, kama wengi wenu mnavyokumbuka, Bwana akinionyesha, miaka sita kabla hajazaliwa. Daktari alisema, “Isingewezekana. Asingelizaliwa.” Lakini Bwana alisema itakuwa hivyo, kwa hiyo Joseph akaja moja kwa moja, bila kuchelewa. Na kwa hiyo sisi. . . Alikuwa na umri wa miaka miwili hivi wakati huo, ama mitatu.

¹⁸ Ninakumbuka ile asubuhi tulipoenda huko hotelini. Joseph aliniangalia wakati nilipokuwa nikivaa nguo niende kwenye kiamshakinywa pamoja na Ndugu Evans. Sikuwa nimekutana naye bado. Nami nikamwambia mke wangu, “Meda, unajua, mpenzi, ya kwamba, mtu huyu tutakayekutana naye. . .” Nikaeleza sifa zake. Nikasema. . . Yeye pamoja na mke wake. “Nami niliona ono juu yake asubuhi ya leo. Yeye anapenda kuvua samaki, ila yeye ni mvunja sheria.” Kisha nikasema, “Ni—ni—ninamwona akifanya jambo fulani asilopaswa kufanya.” Nikasema, “Sijui kama nimwambie ama nisimwambie.”

“Vema,” mke wangu akasema, “afadhali uwe mwangalifu.”

Nikasema, “Nitakuwa mwangalifu.”

¹⁹ Na kwa hiyo maskini Joseph akaamka kitandani. Akasema, “Baba, je! unajua David atapatwa na ajali kwenye pikipiki yake?”

Nami nikasema, “Ati nini, mwanangu?” Mama yake akashika jambo hilo.

Kasema, “Daudi.”

²⁰ David Wood ni jirani yangu. Yeye alikuwa Shahidi wa Yehova, na mguu wake ulikuwa—ulikuwa na polio, nayo ikakunja mguu wake chini yake. Na kwenye mmoja wa mikutano, baba yake na mama yake walimleta kule. Ndipo Bwana Yesu akafunua yote kumhusu yeye, kwamba alikuwa nani, na akamwambia asimame kwa miguu yake. Iliponywa,

na papo hapo mguu wake ukatoka, mzima. Na baba yake ni kondrakta. Alimpa Bwana Yesu moyo wake wakati huo, naye akahama akawa jirani yangu, na amekuwa akiishi hapo kwa miaka kadhaa iliyopita. Naye mvulana huyo, isipokuwa akumbuke, hata hajui ulikuwa ni mguu upi ulio—uliodhurika.

²¹ Wako watu wanaoketi hapa, usiku wa leo, wanaomjua mvulana huyo. Ni wangapi wenu hapa wanaomjua David Wood? Kuna wengi wenu, hakika, ambao—ambao—ambao wamemwona mvulana huyo.

²² Basi Joseph akasema, “Ndio kwanza nimwone David akijeruhiwa akiwa juu ya pikipiki, huko chini kwenye unjia karibu na jengo la shule.”

²³ Vema, nikawazia. Siku chache kabla ya jambo hilo, alikuwa ameniambia kwamba alikuwa akimngojea dada yake mdogo arudi nyumbani. Alikuwa kwenye baiskeli yake ya watoto. Akasema, “Baba, niliona . . .” Kasema, “Je, yupo Mtu *kule* juu, ambaye ana m—mkono mkubwa *hivi*?”

Nami nikasema, “Sijui. Kwa nini?”

²⁴ Akasema, “Niliangalia juu.” Kisha kasema, “Nilikuwa nikielekea barabarani, juu ya baiskeli yangu ya watoto.” Kisha kasema, “Nikaona mkono mkubwa mno, ulionekana kama ni mkono wa Yesu, ulikuwa ukinizua nisiingie barabarani.”

²⁵ Vema, hatukuwazia mengi juu ya jambo hilo. Lakini wakati alipotwambia unabii huu, ya kwamba David atajeruhiwa kwenye pikipiki, hilo kwa namna fulani lilikuwa ni la ajabu kwangu. Na unajua, tulikuwa nyumbani siku tatu. . . Naye akaniambia ni mguu upi utakaojeruhiwa, “Wa mkono wa kuume. Itazirarua nguo zake, itajeruhi upande wake wa kuume.”

Tukasema, “Uliota jambo hilo jana usiku, Joseph.”

²⁶ “La, la.” Hakuota. Kasema, “Ni—nimemwona Da-da sasa hivi amejeruhiwa.” Unaona? Vema, nilifikiri alikuwa akicheza tu.

²⁷ Siku tatu baada ya sisi kufika nyumbani, David aliruka kwenye pikipiki. Mvulana fulani alitoka Louisville kwa pikipiki. Alishuka kwenda barabarani, na moja kwa moja kwenye mahali pale pale akaiangukia pikipiki, na kuujeruhi mguu wake sehemu yote kwenda juu, mkono wa kuume.

²⁸ Na hiyo ni ile si—siku tu niliyokutana na Ndugu Evans. Kwa hiyo baada ya kuzungumza naye, na kuona ya kwamba alikuwa tu ni ndugu mzuri mkazi wa Kusini, nilisema, “Ningetaka kukuuliza jambo fulani.” Nikasema, “Unashuka kwenda kuvua samaki katika kile kinamasi huko chini mahali fulani. Ilionekana kana kwamba ni Florida, kwangu mimi.”

Akasema, “Ndio.”

²⁹ Nikasema, “Hivi karibuni tu ulikuwa na gunia lililojaa samaki. Hukupaswa kuwa na wengi namna hiyo,” Nikasema. Naye akasema, kwa namna fulani...Uso wake ukawa mwekundu; akainamisha kichwa chake. Nami nikasema, “Ulikuwa ukitoka, wewe na mvulana wako, nawe ukawaficha samaki hao mara tatu, maana ulimwona bwana nyama kwa mbali. Ulifikiri alikuwa ndiye.”

³⁰ Akasema, “Naam, bwana. Hiyo ni kweli.” Uso wake, mwekundu sana, yeye na mke wake.

Nikasema, “Kuna ninii tu . . .”

Akasema, “Sa—sa—samahani. Ha—haikunipasa kufanya hivyo.”

Nikasema, “Lakini hakika ningetaka kwenda kuvua samaki kule chini.”

Vema, akanichukua. Tukashuka tukaenda kule.

³¹ Na kwenye, tulipokuwa tukirudi, kuna nyoka tu wabaya sana kule nyuma kwenye hao, ngwena, na mamba, nyoka, na kila kitu, kule nyuma. Ni wabaya kuliko wanyama katili wa Arizona Gila. Wana kile wanachoita nyoka mchacharisha wa ardhini, maskini jamaa mdogo, naye ni—ni jamaa mchoyo. Naye ndugu yake aliumwa na mmoja, yapata miezi mitatu ama minne kabla ya hapo, naye alikuwa angali ana kalibu mguuni mwake, na bambo juu yake, kwa miezi kadhaa. Naye akalazwa hospitalini, hawakujua kama angeishi ama angekufa; ndugu yake mdogo.

³² Kwa hiyo mimi na Ndugu Evans tulikuwa tumerudi kule, nami nilikuwa nikivua samaki. Loo, nilikuwa na siku nzuri sana.

³³ Ninapenda tu kuvua samaki. Mimi, mimi ndiye mvuvi hafifu sana ulimwenguni, bali nina kiongozi mzuri: Yeye. Naye huniambia mahali walipo, na kwa kawaida ninawapata.

³⁴ Nami nilipata wazuri siku hiyo. Nami ningemning'iniza mmoja mkubwa sana, namna ya samaki mkubwa mno, karibu ratili kumi ama kumi na moja, nafikiri. Nisingeweza kumshikilia. Na chambo kidogo cha nyukibambi alichokuwa ametoa mdomoni mwake. Na mdomo wake karibu namna *hiyo*, na huyo nyukibambi mdogo karibu namna *hiyo*. Angeweza kuinuka, kukitupa tu kutoka mdomoni mwake. Lakini alikuwa na hasira sana. Nilimrusha ndani tena, kisha akashikwa kwa mara ya tatu.

Ndipo Ndugu Evans akasema, “Loo, mshike, Ndugu Branham.”

³⁵ Kwa hiyo nilikuwa nikirusharusha pale kwa fimbo hii, nikijaribu kumfanya samaki huyu mkubwa ashambulie tena, na mwingine, loo, kitu fulani, jamaa mkubwa mno akaipiga, nami kwa namna fulani nikamfanya achoke kabisa. Nikamtoa kwenye mayungi-maji mpaka akawa anakaribia ukingoni.

³⁶ Ndugu Evans akiwa ameketi pale, alikuwa amelowesha miguu yake. Alikunja tu miguu ya suruali yake ndefu, na hakuwa na viatu. Akasema, “Hebu kidogo.” Hariri nyororo na kadhalika zilikuwa zimekunjwa, namna hiyo. Kasema, “Nitampata.”

³⁷ Nikasema, “Usijali. Nitamvuta nimwingize, haidhuru. Akichopoka, tuna wengi.”

³⁸ Kwa hiyo nikaanza kumvuta ndani, namna hiyo. Kasema, “Nitampata.” Alipokuwa akitoka, nyoka-mtatarika mdogo wa ardhiini akamuuma, mara tu alipotoka, moja kwa moja juu ya mguu, moja kwa moja juu ya mfupa wa tindi ya mguu.

³⁹ Sijapata kusikia mta—mtazamo kama huo usoni, ama kusikia kilio kama hicho. Akatoka kule nje, na akishika mikono yake namna *hiyo*, na kusaga meno yake. Nikaangalia, na kulikuwa na kidogo tu, karibu umbali huu ambapo meno ya huyo nyoka yalikuwa yamemuuma moja kwa moja mguuni mwake.

⁴⁰ Sasa, wewe ndiwe mtu mgonjwa sana ulimwenguni, katika dakika chache tu. Nawe afadhali upate usaidizi ama mahali fulani, maana utakufa. Na hiyo—hiyo—hiyo sumu kweli ni sumu kwa mtatarika wa ardhiini.

⁴¹ Vema, yeye ni mtu mkubwa mno. Nami nilikuwa mdogo sana kumbeba karibu maili mbili hadi kwenye gari, kupitia kwenye mabwawa hayo yenye matope. Nasi tulikuwa tukiwaangalia mamba kila mahali, nami si mjasiri sana karibu nao, haidhuru. Kwa hiyo niliwazia, “Nifanye nini?”

⁴² Na papo hapo kitu fulani kilionekana kunizungumzia, nami nikaona Maandiko ya Bwana, yaliyosema, “Na watavikanyanga vichwa vya nge, na vichwa vya nyoka, wala hakuna kitu kitakachowadhuru.” Ndipo nikawazia juu ya ndugu yake, lakini ndugu yake si mwaminio. Yeye si Mkristo. Bali mtu huyu ni Mkristo. Kwa hiyo alikuwa tu ameukamata na kuushika mguu wake kwa nguvu.

⁴³ Nikaweka mikono juu yake. Nikasema, “Baba wa Mbinguni, tuko katika hali ya hatari, nami si—siwezi kumbeba ndugu yangu. Na zaidi ya hayo, angekuwa mgonjwa sana, kabla sijatoka mahali hapa, sijui kama tungefikia kwenye msaada kwa wakati ufaao ua la. Lakini imeandikwa katika Neno Lako, ya kwamba, ‘Hakuna kitu kitakachowadhuru.’ Na huyu ni mwaminio.”

⁴⁴ Nami nikaona ameacha kuteseka ama kupiga makelele. Na wakati nilipoacha kuomba alikuwa ameketi, akiniangalia, akicheka. Akasema, “Uchungu wote umekwisha.”

⁴⁵ “Vema,” nikasema, “tuendele?” Tukaendelea kuvua samaki. Tukavua siku nzima, usiku huo, karibu saa tano.

⁴⁶ Tulipata samaki wengi sana wakubwa hata, tulipofika ufukoni tena, mbona, walikuwa huko nje wakipiga picha, wakiwaangalia, kufikia usiku sana, karibu saa tano.

⁴⁷ Naye ndugu yake, yule aliyekuwa ameumwa na nyoka, alikuwa na duka la—la vyambo. Naye akaja kule, nasi tukaisimulia hadithi hiyo, tukamwonyesha mahali hapo. Naye ndugu yake akasema, “Ni sawa kuwa wa kidini, bali usiwe mjinga.” Kasema, “Wewe nenda hospitalini upesi uwezavyo, na ukapewe huduma ya kwanza.”

⁴⁸ Ndugu Evans akasema, “Kama Mwenyezi Mungu amenilinda tangu saa tano asubuhi ya leo mpaka saa tano usiku wa leo, hilo latosha.” Kamwe hata hakupata maumivu mengine.

⁴⁹ Waweza kusimama tu, Ndugu Evans, kusudi watu wapate kuona ni nani niliyekuwa nikizungumza habari zake? Huyu ndiye ndugu huyo pale pale. Ndugu Dauch...

⁵⁰ Na, loo, Yeye ni Mungu popote ulipo. Yeye ni uwepo usioshindwa wa Yesu Kristo. “Tazama, niko pamoja nanyi daima, hata ukamilifu wa dahari.” Naye ni changamoto, kuweka imani yako, wakati wowote utakao, katika Neno Lake, Naye atalitimiza. Sasa ninaninii...

⁵¹ Ni majaliwa kuwa hapa usiku wa leo pamoja na Ndugu yetu mwema Groomer. Nami nimeninii... Yeye amenifuatilia kwa muda mrefu, akaja hapa. Nami ninafikiri tu ni vizuri sana kuwa hapa usiku wa leo, na pamoja na hawa ndugu wengine wazuri, kuweza kukutana na Ndugu Ballard hapa, na wengi wenu. Nasi sote tunatarajia kuwa kwenye kiamshakinywa cha Wafanyabiashara. Na kule chini kwenye—kwenye... Mahali hapo panaitwa jina gani? Ramada. Je! nilitamka hilo sawa? Ramada. Hilo ni la Kihispaniola?

⁵² Ninakumbuka wakati mmoja nilijifunza neno moja katika Kihispaniola, “Oye.” Silitamki hilo sawa tena. Afadhali niliache hilo. Ninamaanisha, “Je! mnanisikia?” Ama kitu kama hicho, “Oye.” [Mtu fulani anasema, “Oye”—Mh.] “Oye.” Ndivyo. “Oye.” Ndilo hilo.

⁵³ Na halafu ile, “Gloria a Dios,” utukufu kwa Mungu. Ndiyo hiyo, “Gloria a Dios.” Ninakumbuka hayo muda mrefu uliopita, kwa hiyo ningali ninasema kwa sauti kuu, “Gloria a Dios.”

⁵⁴ Kwa hiyo sasa, usiku wa leo, kusudi msisimame kwa muda mrefu sana, na—na nina wakati mdogo tu wa ushirika.

⁵⁵ Na samahani, nikisimama hapa jukwaani, nikizungumzia jambo hili na kufurahi, kwa kuwa nina furaha sana kuwa hapa. Nafikiri Mungu anawataka watoto Wake wafurahi. Na—nafikiri tunaweza kulisukuma kupita mipaka, na—na kutokuwa waaminifu kuhusu jambo hilo. Lakini ninaamini ya kwamba Mungu anataka watu wake wawe na furaha kwelikweli, na kushirikiana, tupendane kutoka mioyoni mwetu. “Tukipendana kama vile Mungu, kwa ajili ya Kristo, ama Kristo alivyotupenda.” Nafikiri hiyo ndiyo sababu tunapaswa kuwa Wakristo wenye furaha.

56 Sasa hebu, kabla tu hatujasoma Neno, hebu na tuzungumze na Mwandishi Wake kwa muda mfupi tu, tunapoinamisha vichwa vyetu. Na sasa huku vichwa vyetu vimeinamishwa, wakati sisi, tukiweka kando wakati wetu mfupi wa ushirika wa pamoja sasa, tufahamiane na kuufanya upya ushirika wetu. Nashangaa, katika jengo hili dogo linaloonekana usiku wa leo, aidha nje ama ndani, kama kungekuwako na maombi yoyote yatakayotajwa, na ungeyafanya yajulikane kwa kuinua mkono wako. Mungu tu Ndiye anayejua moyo wako. Mungu na aturehemu. Mungu na aturehemu. Sasa Yeye anajua haja yako. Ni wangapi walio na haja ya kiroho, kwamba mngesainua mikono yenu? Mungu awabariki. Na sasa kwa ajili ya uponyaji wa mwili wenu, inueni mikono yenu, tuone kama kuna wagonjwa wowote. Loo, jamani! Ni ulimwengu ulio mgonjwa, sivyo? Hebu na tuzungumze Naye Ambaye anaweza kuyasahihisha makosa yote.

57 Mwenyezi Mungu, kama vile ulivyomtokea Ibrahimu katika Jina la Mwenyezi Mungu, Wewe ni Mwenyezi Mungu, kutoka milele hata milele. Nasi tunafuraha sana usiku wa leo ya kwamba tuna majaliwa ya kuja Kwako. Tukijua jambo hili, ya kwamba kama tukija katika mwaliko wa Yesu, ya kwamba hapo tuna uhakikisho ya kwamba Wewe unasikiliza. Kwa maana Yeye alisema, "Ombeni Baba lolote katika Jina Langu, nitalitimiza." Sasa, tunaamini hilo, kwa kuwa ni Neno la Mungu. Nasi tuna haja nyingi sana usiku wa leo, Bwana.

58 Tunakushukuru kwa ajili ya kanisa hili, na kwa ajili ya taifa ambalo tungali tunaweza kufanyia mkutano wa aina hii, kwa ajili ya mji ambao usingefunga milango. Tunakushukuru kwa ajili ya mchungaji wake, ndugu yetu wa thamani, na kwa ajili ya halmashauri yote, mashemasi, wadhamini, na washirika wote. Na, Mungu, zaidi ya haya yote, tunakushukuru kwa ajili ya kila msafiri hapa usiku wa leo, wale wanaosafiri pamoja nasi hapa duniani.

59 Tumekuja pamoja, Baba, katika unyoofu wa kuabudu, na tukiamini ya kwamba Wewe utakutana nasi, wala hutakosa kutubariki, na kutujazi haja zetu zilizo ndogo sana. Nawe uliona mikono ya watu hawa kwa ajili ya hali ya kiroho. Ee Mungu, rudisha kila woga na tashwishi, usiku wa leo. Jalia Roho Mtakatifu apate utangulizi.

60 Mungu, tunawaombea wale walio hawawezi, wamekatizwa, hata hawawezi kufurahia maisha, ambao Ibilisi amewatendea uovu na kuwafanya wagonjwa. Jalia wajue, usiku wa leo, ya kwamba kwa mapigo ya Bwana Yesu kila mmoja wetu ameponywa. Jalia tuwe na ujasiri usiku wa leo kupanda kwenda Mbele ya Mungu, kwa imani. Kwa kuwa hakika, Mungu ni Baba yetu, na imani ni mama yetu anayetuzaa, kwa Mungu. Kwa hiyo tujalie, kwa imani ya mama, tuletwe Mbele za Mungu Baba

Ambaye alitoa ahadi hiyo. Na utuokoe na yule mwovu, kama vile Yeye alivyotufundisha kuomba, “Tuokoe na yule mwovu.”

⁶¹ Sasa, Bwana, wabariki wahudumu hawa waliotutembelea. Mkutano wa Wafanyabiashara Wakristo unaokuja, tunauombea huo, kusudi watu wengi wapate kuokolewa. Na tutakapoondoka usiku wa leo, jalia tuweze kusema kama wale waliokuwa wakija kutoka Emau, “Mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani?”

⁶² Bariiki Neno Lako tunapolisoma. “Neno Lako ni Taa,” Taa inayotoa Nuru kutoka duniani kwenda Utukufuni. Na jalia tupande juu kidogo kwenye ngazi hiyo usiku wa leo, Bwana, kwa ajili ya ushirika wetu wa pamoja Mbele za Kristo Yesu. Sasa, Baba, tangu wakati huu, ingia mbele zetu. Chukua Neno la Mungu aliye hai na ulitoe kwa kila moyo ulio na njaa. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

⁶³ Sasa, ninyi ambao mnapenda kuchukua mafungu ya maneno, ama mnaotaka kusoma katika Maandiko pamoja nasi, kama mtafungua katika Biblia zenu katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 1, ninataka kusoma sehemu kubwa ya Neno, kutoka katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 1. Na sasa tutaanzia kwenye kifungu cha 15 cha Yohana Mtakatifu mlango wa 1.

Yohana alimshuhudia, akapaza sauti yake akasema, Huyu ndiye niliyenena habari zake ya kwamba, Ajaye nyuma yangu amekuwa mbele yangu; kwa maana alikuwa kabla yangu.

Kwa kuwa katika utimilifu wake sisi sote tulipokea, na neema juu ya neema.

Kwa kuwa torati ilitolewa kwa mkono wa Musa; neema na kweli zilikuja kwa mkono wa Yesu Kristo.

Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote, Mungu Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, . . . ndiye aliyemfunua.

Na huu ndio ushuhuda wake Yohana, Wayahudi walipotuma kwake makuhani na Walawi kutoka Yerusalemu ili wamwulize, Wewe u nani?

Naye alikiri, wala hakukana; alikiri kwamba, Mimi siye Kristo.

Wakamwuliza, Ni nini basi? U Eliya wewe? Akasema, Mimi siye. Wewe u nabii yule? Akajibu, La.

Basi wakamwambia, U nani? Tuwape ma—majibu wale waliotupeleka. Wanenaje juu ya nafsi yako?

Akasema, Mimi ni sauti ya mtu aliaye nyikani, Inyosheni njia ya Bwana! Kama vile alivyoenenda nabii Isaya.

Nao wale waliotumwa walikuwa wametoka kwa Mafarisayo.

Wakamwuliza, wakamwambia, Mbona basi wabatiza, ikiwa wewe si Kristo, wala Eliya, wala nabii yule?

Yohana akawajibu akisema, Mimi nabatiza kwa maji. Katikati yenu amesimama yeye msiyemjua ninyi.

Ndiye yule ajaye nyuma yangu, ambaye mimi sistahili kuilegeza gidamu ya kiatu chake.

Hayo yalifanywa huko Bethania ng'ambo ya Yordani, alikokuwa Yohana akibatiza.

Siku ya pili . . . (Samahani) . . . Yohana amwona Yesu anakuja kwake, akasema, Tazama, Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu!

Huyu ndiye niliyenena habari zake kwamba, Yuaja mtu nyuma yangu, ambaye amekuwa mbele yangu; kwa maana alikuwa kabla yangu.

Wala mimi sikumjua; lakini kusudi adhihirishwe kwa Israeli ndiyo maana mimi nalikuja nikibatiza kwa maji.

Tena Yohana akashuhudia akisema, Nimemwona Roho akishuka kama hua kutoka mbinguni; naye akakaa juu yake.

Wala nami sikumjua; lakini yeye aliyenipeleka kubatiza kwa maji, huyo aliniambia, Yeye ambaye utamwona Roho akishuka na kukaa juu yake, huyo ndiye abatizaye kwa Roho Mtakatifu.

Nami nimeona, tena nimeshuhudia ya kuwa huyu ni Mwana wa Mungu.

Tena siku ya pili yake Yohana alikuwa amesimama pamoja na wawili katika wanafunzi wake;

Na akamtazama Yesu akitembea . . . kasema, Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu!

Na wale wanafunzi wawili wakamsikia akinena, wakamfuata Yesu.

Na ndipo Yesu aligeuka, akawaona wakimfuata, akawaambia, Mnatafuta nini? Wakamwambia, Rabi, (maana yake, Mwalimu), unakaa wapi?

Akawaambia, Njoni, . . . mtaona. Wakaenda, wakaona akaapo, wakakaa kwake siku ile: Nayo ilikuwa yapata saa kumi.

Andrea, nduguye Simoni Petro, alikuwa mmoja wa wale wawili waliomsikia Yohana na kumfuata Yesu.

Huyo akamwona kwanza Simoni, ndugu yake mwenywe, akamwambia, Tumemwona Masihi (maana yake, Kristo).

⁶⁴ Bwana na aongeze Baraka Zake kwenye kusoma huku kwa Neno Lake. Na sasa, kwa shauku kubwa mno, hebu niwakumbushe kwa dakika chache so—somo dogo, kwamba kama ningeliliita hilo. Nikiketi kwenye dawati, muda mfupi uliopita, yapata saa tisa ama kumi alasiri ya leo, nikisoma, hili lilinigusa. Na kutoa somo kwenye jambo hili, ninataka kuchukua hili, maneno haya mawili: *Kushawishika Kisha Kuhusika. Kushawishika Kisha Kuhusika.*

⁶⁵ Sasa, tunaishi katika wakati mbaya sana. Tunaishi katika wakati wa ukungeufu mkubwa mno. Tunajua jambo hilo. Tunafahamu.

⁶⁶ Jana jioni nilikuwa nikihubiri juu ya somo la Kudhania, huko chini kwenye kanisa hilo lingine. Watu wakichukua namna fulani ya kitu fulani, nao wakidhania tu wao ni Wakristo. Nalo neno *kudhania*, kama tulivyolielezea jana usiku, linamaanisha “kuthubutu bila mamlaka.” Na watu wengi kupita kiasi wanathubutu siku hizi. “Vema,” wanasema, “nilifanya hivi na vile. Nilijiunga na kanisa. Nili—nilizamishwa majini. Nadhani mimi ni Mkristo.” Hilo halitafaa kitu. Hilo, huwezi kulidhania. Inakubidi kuwa na hakika ndivyo ulivyo. Unaona? Wewe, inakupasa kujua kweli ya kwamba wewe ni Mkristo. Kwa hiyo, leo, ninajisikia, mbele za . . .

⁶⁷ Taifa letu lina wafuasi wengi wa Kikristo kuliko taifa hili lilivyopata kujua. Lakini je! ulijua, mwaka jana, kulingana na takwimu, ya kwamba hakujakuwa na . . . hakuna seminari. Moja lililingana tu kidogo na mwaka uliopita. Lakini kila seminari nyingine, ama shule, ama shule ya Biblia, ilishindwa kufikia kiwango chake cha wahuduma. Ambapo vijana, walio na miito maishani mwao, kwenda hudumani na kadhalika, wanaenda kwenye mafunzo yao, na kadhalika, jinsi walivyokuwa wakisimama mstarini wapate kuandikishwa kwenye shule hizo, na sasa ni vigumu kwako kuwashawishi waingie. Kuna kasoro mahali fulani. Unaona? Ninaamini, kwa moyo wangu wote, bila ninii yoyote, nikitumaini sisemi jambo lolote baya, bali ninaamini ni kwa sababu ya kutokuwa na shauku, kuhusika, hawahusiki vya kutosha. Kuna kuhusika kwingi mno kuhusu kutengeneza bomu la atomiki, kuhusika kwingi mno kuhusu ni nani atakayefika mwezini kwanza. Na—nami sijali kuhusu kufika mwezini. Ninataka kufika Mbinguni, ndiko ninakotaka kwenda.

⁶⁸ Mwajua, hao daima wanapiga makelele kuhusu “Sisi ndio wa kwanza kumpeleka mtu angani.” Urusi inaendelea kutupigia makelele, “Tulimweka mtu angani.”

⁶⁹ Mbona, tumekuwa na mmoja angani kwa muda wa miaka elfu mbili. Hakika. Sisi, wao . . . ? . . . Wako—wako nyuma sana, wako maili elfu mbili nyuma yetu. Tulikuwa na mtu angani huko nyuma, sasa, miaka elfu mbili iliyopita, aliyefufuka

kutoka kaburini, na yuko angani, na kotekote, kila mahali. Hakika. Kwa hiyo huyo ndiye tunayemtazamia. Yeye atatupeleka mahali aliposema. “Nyumbani mwa Baba Yangu kuna makao mengi, nami nitaenda kuwaandalia mahali.” Mahali fulani ng’ambo ya anga huko ng’ambo, sijui, bali yeye atarudi aje kutuchukua. Jambo ndilo hilo. “Msifadhaike mioyoni mwenu, wala msioCOPE.” Loo, ninapenda jambo hilo. Hilo linanifanya tu nijue, ya kwamba, “Kuna makao katika ule Mwamba mahali fulani, huko mbali sana mbele ya kilele cha mlima,” kama vile mshairi alivyosema.

⁷⁰ Sasa, ukengeufu huu ni kutokuujali Mwili wa Kristo. Ninaamini ya kwamba labda jambo linalofaa halijaelezewa. Wanafunzi wengi sana vijana ambao wangepachukua wito maishani mwao, wanaona kushindwa kwingi sana hapa nje, na kweli wanaona ya kwamba utaratibu na mpango wa siku hizi umeshindwa. Sio. . . Kristo hajashindwa, bali mfumo tulio nao ambao tumeubuni umeshindwa. Mpango wa Kristo haujashindwa. Lakini mfumo wa watu umeshindwa. Sasa, Kristo ana mpango tunaopaswa kuingia ndani yake.

⁷¹ Sasa, tungeweza kudumu muda mrefu kwenye Maandiko haya machache na kadhalika niliyotaka kuyarejea. Lakini kwa kuharakisha, hebu na tuanze sasa na tuanze nyuma kwenye Kitabu cha Isaya, na tuanze na Yohana alipoitwa kwanza “sauti ya mtu aliaye nyikani,” miaka mia saba na kumi na miwili kabla ya kuzaliwa kwake.

⁷² Na wakati Zakaria, baba yake, kuhani katika siku yake, alipokuwa mhudumu katika hekalu la Bwana. Naye pamoja na mke wake, Elisabeti, walikuwa wenye umri mkubwa sana. Ndipo Roho Mtakatifu akamjia Zekaria na kumbariki, na kumwambia kuhusu mtoto huyu, kama sote tujuavyo. Lakini hapana budi lilikuwa ni jambo la kushangaza, na hisi katika moyo wa huyo mume na mke wenye umri mkubwa, wakati mwana huyu aliyeahidiwa alipowasili. Na, matamshi yake, alikuwa bubu mpaka wakati alipompa jina lake, kulingana na Neno la Mungu. Unaona?

⁷³ Neno la Mungu ni kamilifu sana. Lakini kwa sababu yodi moja wala nukta moja kamwe haiwezi kupita, haiwezi kupita hadi imetimizwa. Yesu anakuja, Naye anakuja kwa ajili ya Kanisa lisilo na waa wala kunyanzi. Wala hata Neno moja wala yodi moja ya Hilo haitashindwa. Kanisa litakuwa katika hali hiyo wakati Yesu atakapokuja. Wao wanatungojea.

⁷⁴ Sasa, angalia ya kwamba Zekaria na Elisabeti, kwa kuwa walikuwa wenye umri mkubwa, walijua ya kwamba wasingeweza kuishi muda wao wa wakati, muda mrefu kutosha kuona mwanao, kile Mungu alichomwekea. Ila walijua ya kwamba Mungu alikuwa pamoja naye, kwa maana Roho Mtakatifu alikuwa ameahidi ahadi hiyo, nao walijua ya kwamba

Mungu angemlinda mtoto wao. Sasa, kulingana na historia hiyo pale, wao walikufa wakati yeye alipokuwa na umri wa miaka tisa.

Na, Yohana, jinsi watu hawa walivyo wa ajabu.

⁷⁵ Sasa, ilionekana kana kwamba Yohana, akiwa ametoka kwenye nyumba ya kuhani, ya kwamba yeye akiwa ni mtu wa kidini, na akijua ya kwamba kulikuwa na wito maishani mwake, angalienda moja kwa moja shuleni na kuwa kuhani kama baba yake. Sasa, hayo yangukuwa ndiyo mawazo ya kawaida.

⁷⁶ Wakati mvulana anapopata wito maishani mwake, jambo la kwanza wanalowazia ni kukimbia kwenda kwenye siminari mahali fulani, unaona, wakimbilie shuleni ama kitu kama hicho, unangojea mpaka utakapopata digrii zako, na kadhalika, kabla hujahubiri.

⁷⁷ Na, sasa, Yohana alifanya tu kinyume cha hilo, badala ya kwenda kwenye shule ambayo baba yake alitoka. Yeye alijua kulikuwa na wito maishani mwake. Naye alijua kwamba alikuwa amtanga-... alikuwa amtambulishie, kwa ulimwengu, Masihi, kwa sababu alikuwa amtangulie. Wala kusingekuwako na kosa kwenya jambo hilo.

⁷⁸ Kwa hiyo, badala yake, yeye alijua kwamba kama alishuka akaenda kule shuleni na kuwaambia, “Wengi wenu hamfahamu jambo hilo hapa, bali mimi ndiye niliyezaliwa na akina Zekaria, yule kuhani, aliyepata mafunzo yake hapa katika shule hii ya thiolojia. Nami nime-... Mimi... Mnamjua mama yangu, mwanamke mwenye haki, nanyi mnajua kwamba mimi ni nani. Kwa hiyo nimeshuka kuja hapa, ‘askofu, askofu mkuu,’ kadhalika, ku—kujifunza jinsi Masihi huyu atakavyokuwa, kwa sababu itanibidi kujua jinsi atakavyokuwa. Itanibidi kuwa na hakika, kwa sababu Yeye atakuwa ni Mwanadamu. Itanibidi kujua jinsi alivyo, kusudi niweze kweli kumtambulisha kwa ulimwengu.”

⁷⁹ Sasa, hiyo ni huduma muhimu. Ndugu zangu, mwajua, tunayo huduma ile ile. Kweli. Ni kuwajulisha kweli, watu, yule Masihi.

⁸⁰ Kwa hiyo yeye alijua ya kwamba kama angalishuka kwenda huko chini kwenye shule hiyo, ya kwamba kila mtu angekuwa na wazo tofauti kuhusu jambo hilo, na lingesababisha tu mchafuko.

⁸¹ Lakini Yohana, kwenye umri wa miaka tisa, alienda nyikani, apate kuwa peke yake na Mungu, kusudi asifanye kosa. Alitaka kujua jinsi Masihi huyu angekuwa, jinsi ambavyo angempata, jinsi angeonekana, kusudi aweze kumtambulisha. Nasi tunaona ya kwamba, badala ya kwenda kuchukua digrii zake zote na kutokea kama kuhani jinsi baba yake alivyokuwa, na kufuata nyayo za baba—baba yake, alienda mbali sana na shule kadiri alivyoweza kwenda, moja kwa moja hata nyikani, akiwa peke yake pamoja na Mungu.

⁸² Sina neno dhidi ya shule hizo. Sina neno dhidi ya hizo hata kidogo. Hizo ni sawa kabisa. Lakini mara nyingi, baada ya wewe kupata digrii yako shuleni, ungali unapaswa kwenda huko nyikani mahali fulani, kupata mapenzi ya Mungu. Hilo ni sawa. Ni kweli.

⁸³ Sasa, Yohana, akishika ofisi hii kuu, alienda moja kwa moja nyikani, naye alikuwa huko tangu umri wa miaka tisa mpaka alipokuwa na umri wa miaka thelathini, nyikani.

⁸⁴ Unaweza kuona jinsi alivyozungumza; yeye alikuwa mtu wa nyikani. “Loo, enyi uzao wa nyoka.” Unaona? Alikuwa amewazoea nyoka nyikani. Unaona? Yeye... Unaona? “Loo, shoka limewekwa kwenye shina la mti.” Unaona? Alikuwa mtu wa nyikani. Unaona? A—alihubiri jinsi alivyokuwa ameishi, katika mazingira aliyoishi. Naye alitoa hiyo mifano ya vitu ambavyo alikuwa amejifunza huko nyi—nyikani.

⁸⁵ Sasa, kwa nini Yohana alikuwa na hakika jinsi hii? Je! Mliona, yeye hakusema, “Labda huyu ndiye”? Alisema, “Tazama, huyu ndiye!” Angekuwaje na uhakika jinsi hiyo?

⁸⁶ Sasa hebu tusome kifungu kingine. Kifungu cha 26, nimekiandika hapa. Ninataka kuona kile tutakachopata kutoka kwenye kifungu hiki cha 26 hapa.

Yohana akawajibu akisema, Mimi nawabatiza ninyi kwa maji. Katikati yenu amesimama yeye msiyemjua ninyi.

⁸⁷ Angalia. Yohana alijua. Yohana alikuwaje na uhakika sana ya kwamba moja kwa moja miongoni mwa kundi hilo mahali fulani, alikuwako yule Masihi, amesimama pale wakati huo? “Katikati yenu amesimama Mtu, msiyemjua, naye Ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu.” Unaona? Yeye alimjua. Kwa nini? Kwa sababu wakati ulikuwa umewadia.

⁸⁸ Ndugu, wakati umewadia. Ni muhimu kwa Mkristo, si kujiunga tu na kanisa, wala kutegemea kitu fulani, ushawishi fulani, mihemuko fulani, ama kitu kama hicho, bali kuwa na hakika ya kwamba uko sawa.

⁸⁹ Sasa, kuna mengi sana leo tuliyo nayo. Wengine wanaridhika na masomo. Wengine wanaridhika na kujifunza kanuni za imani. Wengine wanaridhika na hisia ndogo za ajabu. Wengine wanaridhika na mambo mbalimbali. Ambalo, sina neno dhidi ya jambo hilo. Hilo ni sawa. Bali hilo silo ninalosema habari zake. Unaweza kuwa na hilo bila kuwa na kile kitu halisi. Unaona?

⁹⁰ Na hivyo ndivyo tunavyojaribu kusema. Hatuna budi kuwa na uhakika, kwa sababu wakati umekaribia, kwa ajili—kwa ajili ya ubatizo wa kweli wa Roho Mtakatifu. Yeye aliahidi angemmwaga katika siku za mwisho.

⁹¹ Sasa, kuna watu wengi sana wanaosema, “Kama ukitetemea. Funga macho yako. Fanya mambo ya kila namna,

na upate mhemuko.” Unapata roho, rafiki. Lakini kama maisha yako hayalingani na yale unayokiri, basi roho uliyo nayo ina kasoro. Unaona? Na ni kweli. Unaona?

⁹² Wewe, huna budi kuwa na hakika. Roho Mtakatifu ataleta maisha matakatifu, hiyo ni kweli, na kama shauku hiyo imo moyoni mwako. Kama itakulazimu kujilazimisha daima, kujaribu kujitahidi na kufanya yaliyo mema, na ulimwengu ungali unaona njaa ndani yako, basi kuna kasoro fulani. Unaona? Roho Mtakatifu, ndani yako, hatauonea ulimwengu njaa. Atamwonea Mungu njaa. Kama ni vigumu kwako kwenda kanisani, na kujitahidi kuja wakati kanisa limefunguliwa, roho huyo ana kasoro. Anajaribu kukuweka mbali na Mungu. Roho wa Mungu atakuelekeza moja kwa moja kanisani kila wakati mlango utakapofunguliwa kwa ajili ya ushirika. Naam, bwana. Unaona? Kwa hiyo huna budi kuwa na uhakika wa jambo hili sasa. Wakati umekaribia.

⁹³ Sasa, Yohana alijua ya kwamba wakati ulikuwa umekaribia, kwa hiyo basi yeye alisema, “Yupo Mtu anayesimama hapa, mahali fulani, katikati yenu, Ambaye hamumjui.” Wala yeye naye hakumjua, wakati huo, la sivyo angalisema, “Huyu *hapa*, ama yule *pale*. Ndiye Yule anayesimama *pale*.”

⁹⁴ Lakini Yohana, kama angalienda shuleni, labda angaliweza kuonyesha hamsini.

⁹⁵ Lakini, unaona, Yohana alikuwa ameenda kwenye shule tofauti. Yohana alikuwa mbele za Mungu. Yohana alikuwa amemfunulia, kwa Mungu, Neno la Mungu hasa, jinsi ambavyo Masihi angekuwa. Kwa hiyo yeye alikuwa akingojea kuona ishara ya Masihi. Alitaka kuona Masihi alikuwa wapi. Mungu aliahidi, “Nitamthibitisha huyo Masihi kwako.”

⁹⁶ Ninawaambia sasa, kama ukitaka Maandiko kwa ajili ya jambo hilo, itakuwa ni ishara ya Maandiko. Kifungu cha 33, hebu tuchukue kifungu cha 33 hapa na kukisoma. Sasa angalieni.

Nami namjua, sikumjua: . . .

. . . sikumjua; lakini yeye aliyenipeleka kubatiza kwa maji, huyo aliniambia, Yeye ambaye utamwona Roho akishuka na kukaa juu yake, huyo ndiye abatizaye kwa Roho Mtakatifu.

⁹⁷ Unaona? Huyo hapo Mungu, anataka, anataka kuhakikisha ya kwamba hakuna kuchanganyikiwa juu ya jambo hilo. Mungu alisema, “Yohana, nitakupa ishara. Halafu utakapoona ishara hii juu Yake, hiyo itathibitisha ya kwamba Huyo ndiye.”

⁹⁸ Yohana akasema, “Yeye anasimama huko nje mahali fulani, bali si—simjui bado.”

⁹⁹ Lakini mara alipomwona Ro—Roho akishuka na kukaa juu Yake, hakuna mtu mwingine aliyemwona ila Yohana. Hebu

wazia tu jambo hilo. Roho Mtakatifu alishuka, katika umbo la Hua, na kukaa juu ya Yesu, wala hakuna mtu aliyemwona ila Yohana, maana hiyo ahadi ilifanywa kwa Yohana.

¹⁰⁰ Sasa, kama kuna asiyeamini hapa ambaye haamini katika ubatizo wa Roho Mtakatifu, unasema, “Siamini jambo hilo kamwe,” kamwe hutajua jambo lolote kuuhusu. Unasema, “Siamini katika uponyaji wa kiungu. Siwezi kuona ni kweli.” Hakika huwezi. La, bwana. Lakini, yeye aaminiye, ni kwa ajili ya waaminio. Yule aliye na njaa moyoni mwao kumwona Mungu, huuona. Hakuna mtu. . .

¹⁰¹ Hao watu waliokuwa pamoja na Paulo, hawakuiona ile Nuru ikining’inia pale juu ya Paulo. Hawakuiona hiyo nuru. Lakini ilikuwa ha—halisi sana kwa Paulo, hata, iliyapofusha macho yake. Angavu sana, hata iliyapofusha macho ya mtu mmoja, aliyesimama, akiiangalia, na hao wengine waliosimama pale wasingeweza hata kuona. Kwa hiyo, unaona, inatumwa kwa hao wanaoamini na wako tayari kuipokea.

¹⁰² Wale wanafalaki, Mamajusi kutoka mashariki, waliifuata ile Nyota kwa muda wa miaka miwili, kote kuvuka Mto Tigresi, na kupitia kwenye nyanda. Nao walitoka huko mbali Arabuni, wakaingia India, wakashuka wakaja Yerusalemu, wakiifuata ile Nyota. Nayo ilipita juu ya kila chumba cha kuchunguzia, wala hakuna yeyote wao aliyehandika jambo lolote kuihusu; hawakuiona. Lakini *wao* waliiona.

¹⁰³ Kwa hiyo ninaamini, usiku wa leo, ya kwamba Roho Mtakatifu yuko hapa. Yuko hapa kwa wale waliokusudiwa kumpokea, ambao wanamwamini, wanaomngojea. Yuko hapa kunyosha kila moja ya hizo shida za kiroho. Yuko hapa kumponya kila mgonjwa aliyeko. Yuko hapa. Lakini inakubidi kuja na kuingia katika—mazingira Yake, na jinsi ya kumpokea. Inakupasa kuja, si kwa kuchochewa kimhemuko. Inakupasa kuja juu ya msingi wa kuamini ahadi aliyoifanya Mungu. Hilo latosha. Hilo ndilo latosha.

¹⁰⁴ Yeye alikuwa akingojea kuona hiyo ishara, halafu alikuwa . . . angeweza kumtangaza. Naye alimtangaza.

¹⁰⁵ Sasa, siku ya pili, Yohana alimwona tena, naye akasema, “Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu.” Yeye alikuwa na hakika. Alijua huyo alikuwa Ndiye.

Wao walisema, “Unajuaje?”

¹⁰⁶ Akasema, “Yeye aliyenituma huko nyikani kubatiza kwa maji, alisema, ‘Yeye ambaye utamwona Roho akishuka, na kukaa juu Yake, Huyu ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto.’”

¹⁰⁷ Kulikuwa na wawili wa wanafunzi Wake waliosimama pale, nao wakamfuata Yesu. Na wakati sisi. . . Walikuwa ni Filipo, Andrea. Lakini wakati walipofika kwa. . . Walisema,

“Rabi, unakaa wapi? Tungetaka kujua mahali unapokaa. Sasa, tumekuwa tukimsikiliza nabii aliyesimama hapa chini mtoni. Naye amekuwa akitwambia sasa, kwa muda wa miezi sita, ya kwamba Masihi yuaja, naye angemtambua. Sasa, tunamjua nabii huyo kwamba ni mtu mwenye haki. Tunaamini kwamba Yeye ni nabii. Yeye—Yeye ni nabii aliyethibitishwa. Tunajua ni nabii. Naye anasema kwamba Wewe ndiye huyo Masihi. Sasa, tungetaka kujua mahali unapokaa.”

Ndipo akasema, “Njoni, mwone.”

¹⁰⁸ Nao wakaingia wakakaa usiku kucha pamoja Naye, kwa maana ilikuwa ni alasiri sana. Je! uliona, walikaa pamoja Naye usiku huo. Na kesho yake asubuhi, Andrea alikuwa ameshawishika kabisa hata alitaka kumtafuta ndugu yake. Unaona?

¹⁰⁹ Sasa, hiyo ndiyo njia pekee ninayoona kwa ajili ya kuweko na kuhusika kanisani, na huko nyuma miongoni mwa watu, ni kukaa muda mrefu vya kutosha mpaka umeshawishika ya kwamba mpango huo ni kweli, na ni Mungu; wala si udanganyifu wa kiakili, ama mhemuko, ama—ama saikolojia, ama kujifanya kwa namna fulani. Ni ubatizo wa Roho Mtakatifu kabisa ambao Mungu aliahidi kuumwaga katika siku ya mwisho.

¹¹⁰ Hiyo ndiyo sababu seminari zinashuka. Wanaona ya kwamba yote wanayopata, kwa njia moja au nyingine, hayaninii... Ni daima kuahidi jambo ambalo hulifikii kamwe. Jambo fulani wanaloahidi, na wanaendelea tu kuahidi, na kuahidi, na kuahidi. Kamwe hulifikii.

¹¹¹ “Lakini ahadi hiyo ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie,” Petro alisema kwenye Siku ya Pentekoste. Sasa, kamwe si kwa ajili ya kundi fulani huko nyuma kabisa, wakati mwingine. Ni leo. Umbali gani? “Kwa wengi watakaoitwa na Mungu Bwana wetu wamjie.” Ishara zilipaswa kumfuata mwamini, kusudi wapate kujua kwamba wao ni akina nani; wakitoa thibitisho lao, ya kwamba walikuwa waaminio.

¹¹² Sasa, Andrea alihusika sana, sana, kwa sababu alikaa pamoja Naye usiku kucha na akashawishika. Ndipo wakati aliposhawishika ya kwamba Yeye alikuwa ni Kristo, basi alihusika kuhusu mtu mwingine.

¹¹³ Nami ninaamini ya kwamba kila mwanamume, kila mwanamke, kila mvulana ama msichana, ambaye anakaa muda mrefu vya kutosha, kwamba umeshawishika ya kwamba Jambo hilo ni kweli, na ni Roho Mtakatifu, unakuwa na mzigo mzito sana moyoni mwako, hata huwezi kusimama kimya na kuwaacha watu hawa wafe namna hii katika aibu na dhambi. Lita uhuzunisha sana moyo wako, utoke hapa nje kwenye mitaa hii. Linafanya hivyo, Mkristo yeyote, kuona watu waliojitolea kabisa kwa dhambi: kunywa pombe,

kucheza karata, kulaani, kutukana, kuvuta sigara. Kila gari unalofuatilia, lina mwanamke aliye na sigara vidoleni mwake, akiwa na moja ya mitindo hii ya kukata nywele kichwamaji, ambayo wana—wanatumia sasa, na upuuzi huu wote wa kawaida. Na maelfu ya hao wanadai kwamba ni Wakristo.

¹¹⁴ Hivi hutambui, ewe rafiki, kwa kuwa niko kwenye jambo hilo, ya kwamba kama vile bibi wa kwanza wa taifa, hivi ulijua Yezebeli alikuwa mke wa mfalme wa taifa hilo pia? Unaona? Hakika. Lakini Eliya alimkemea. Bibi huyo alimchukia, bali yeye alimwambia vile alivyo hasa. Kusema kweli, yeye alikuwa ndiye mchungaji wake. Mwanamke hakutaka kukubali hilo, bali ndivyo alivyokuwa. Hiyo ni kweli. Alimwambia.

¹¹⁵ Sasa, tunaona dhambi yote, na jinsi mambo yalivyo, na inapenya ndani ya moyo wa mtu yeyote. Unawaona watoto wadogo... Mke wangu alikuwa akiniambia asubuhi ya leo. Tulipanda tukaenda kwenye lile kanisa dogo huko mahali pale pengine. Ndugu Williams alitupeleka kule, jana. Naye mke akasema, “Bill, ilikuwa ya kusesimua sana.”

¹¹⁶ Baada ya kuja mitaani na kuwaona wasichana wadogo, si zaidi ya umri wa miaka kumi na miwili, wakitembea kule wakiwa na sigara mikononi mwao, na wavulana wakitoka shuleni, wakiwa wamewakumbatia, mahali pabaya. Watoto, mbona, polisi wanapaswa kushika kitu kama hicho. Vema, huo ni upotovu. Ati nini? Maskini mtoto huyo mdogo, itakuwaje kwake? Huko nje kwenye ulevi mamboleo, na kila kitu, wakinywa pombe, na kucheza karata, na kufanya maovu na wavulana hawa, na hawajapita umri wa miaka kumi na miwili, miaka kumi na minne, na mama zao wabaya vivyo hivyo. Hiyo ni kweli. Na wote ni wafuasi wa kanisa.

¹¹⁷ Yeye akasema, kwenye kanisa hili huko nje jana, “Lilikuwa ni jambo zuri kuona kundi la watoto, wenye umri wa miaka minane ama tisa, wote wakiingia na kwenda madhabahuni na kuomba, halafu wananyakua vitambaa wanaenda kupanguza viti kusudi watu waweze kuingia usiku huo.”

¹¹⁸ Jina la Bwana libarikiwe! Kungali kuna tawi lililosalia, mahali fulani. Kuna masalia ambao Mungu atawakusanya pamoja. Vema.

¹¹⁹ Kushawishika kisha kuhusika. Sasa, Andrea alihusika kuhusu ndugu yake, mara aliposhawishika kabisa ya kwamba huyo alikuwa ni Masihi. Alifanyaje jambo hilo? Alikaa Naye usiku kucha.

¹²⁰ Shida yake ni kwamba, hatuwezi kukaa pamoja Naye dakika tano. “Loo, sina budi kwenda nyumbani. Kipindi fulani cha televisheni kinaendelea. Hatuna budi tu kuona mchezo huo. Siwezi tu kukaa muda mwingine zaidi. Hivyo tu. Sikukikosa hicho muda mrefu sana. Wanaonyesha mfululizo, wajua. Na kwa hiyo si—siwezi...” Naam. Jambo ndilo hilo. A-ha. “Nakwambia.

Si—sina budi tu kufanya jambo *hili*, ama *lile*. Siwezi kufanya *hivi* na kufanya *vile*.” Hakuna wakati.

¹²¹ Loo, ndugu, “Utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu na haki Yake.” Unaona?

¹²² Lakini jambo ni kwamba, basi, hilo linapoteza kuhusika, na baada ya kitambo kidogo umepoteza lote. Umepoteza kila kitu. Huhusiki juu ya jambo lolote wakati huo ila tu maisha yako mwenyewe. Hiyo ni kweli.

¹²³ Tuna husi-...tunahusika sana juu ya kuyajaza makanisa yetu. Tunataka kuona kama sisi...ninii...kama sisi Wapentekoste hatuwezi kuwapata wengi kuliko Wabaptisti. Wabaptisti wanataka kupata wengi kuliko Wamethodisti. Nao kwa furaha wanapiga makelele kwamba wanaongezeka na kuongezeka wakati wote.

¹²⁴ Lakini wao wana nini? Hawana kitu ila wahuni kutoka mle mitaani, wakati hakupaswi kuwa na kitu kinacholekwa kanisani ila kilicho kitakatifu na kilichotakaswa na kutengwa. Si ajabu mwenye dhambi ana wakati mgumu sana. Mbona, hao watu, hata Wapentekoste wetu, wakidhani ya kwamba wao ni Wakristo, wakizunguka na kuchezecheza kwenye ulimwengu, wakikimbilia kwenye sinema na karamu na madansi, wanawake wakikata nywele zao na kuvaa sketi chafu.

Unasema, “Hawafanyi jambo hilo.”

¹²⁵ Shuka uje kwenye kiamshakinywa cha Wafanyabiashara uone kama hawafanyi hivyo, ama la. Kuja kwenye kanisa lolote la Kipentekoste, karibu kila moja, Jumapili asubuhi, uone kama hawafanyi—hawafanyi hivyo. Wanawake wanajikusumiza kwenye nguo dogo na—na kadhalika, wakijiendesha vibaya sana, na kila kitu namna hiyo. Hiyo ni aibu. Mnajua ni aibu.

Mbona, mnasema, “Vema, haikupasi kusema hivyo.” Mimi...

¹²⁶ Ee Mungu turehemu. Mungu na atupe mtu aliye na ujasiri wa kutosha kusema jambo hilo. Ni Biblia. Naam. Hilo ndilo jambo linalopaswa kusemwa. Hakika.

¹²⁷ Vema, mwanamume, mwa—mwa—mwanamume atakayemwacha mke wake afanye hivyo, ni—nina heshima pungufu kwake pia. Angewezaje kuwa Mkristo, wakati anapopaswa kuitawala nyumba yake mwenyewe, kuiweka katika utaratibu? Mbona, ni fedheha. Tunapaswa kurudi kwenye utakatifu, kurudi kwenye yaliyo mema, kumrudia Mungu. Ndivyo ilivyo.

¹²⁸ Lakini wakati unapoona, ulimwengu unapoliona kanisa, sisi tu Wapentekoste tukikiri jambo fulani, ulimwengu unasema hawana. Unaona? Unasema, “Hawana. Wao si tofauti na hao wengine.” Vema, hiyo ni kweli kabisa. Wanasema kweli, kabisa.

¹²⁹ Mnajua, daima tunajaribu kujilinganisha na ulimwengu. Tunajaribu kuushinda. Kama nilivyosema hivi majuzi usiku, mna—mna—mnajaribu kupatana nao kwenye eneo lao. Acha waje kwenye eneo letu. Unaona? Hatutaki kujaribu kupata kile walicho nacho. Tuna kitu fulani ambacho hawawezi kupata isipokuwa wawe mmoja wetu, ambacho sisi, hiyo ni kweli, ni chombo cha Bwana, kumpata Kristo.

Kristo alisema, “Nikiinuliwa juu, nitawavuta watu wote Kwangu.”

¹³⁰ Lakini, unaona, wakati kanisa halifanyi jambo hilo, waliinua...Mnapaswa kumwinua juu, kama vile wimbo ulivyosema, kwa kuishi kama vile Wakristo wanavyopaswa kufanya. Unaona? Lakini badala ya jambo hilo, tunaanza moja kwa moja, mambo yale yale tunayofanya na kadhalika, yanathibitisha ya kwamba hatuna kitu hicho. Unaona? Kwa hiyo ninyi, wao wanadhanja tu jambo hilo, kama nilivyosema hivi majuzi usiku. Usifanye hivyo. Rudi. Usichukue kibadala, maana utakufa.

¹³¹ Pia kumbuka, utakapokufa na nafsi hiyo ikuache, kamwe haibadiliki. La, bwana. Mauti hayaibadilishi nafsi. Yanabadilisha mahali pake pa kuishi, bali ingali ni nafsi ile ile. Kwa hiyo kama haijazaliwa mara ya pili, na ni sehemu ya Roho wa Milele wa Mungu, ilikuwa na mwanzo. Chochote kilicho na mwanzo kina mwisho. Hiyo ndiyo sababu Mungu ndiye kitu pekee kilicho cha Milele.

¹³² Isipokuwa umezaliwa mara ya pili na una Uzima wa Milele (Neno la Kiyunani *Zoe* hapo linamaanisha “Uzima wa Mungu Mwenyewe” ndani yako), utaangamia. Lakini ambapo Uzima wa Mungu umo ndani yako, huwezi kuangamia kadiri Mungu asivyoweza kuangamia, hiyo ni kweli, kwa sababu wewe ni mwana, uzao wa Mungu, nawe una Uzima wa Milele. Loo, hicho ndicho kitu kanisa linahitaji. Ndipo Mungu akiwa ndani yako, basi Yeye anaishi Maisha Yake Mwenyewe kupitia kwako. Unaona? Na hivyo ndivyo tu—tunavyojua ya kwamba sisi ni Wakristo. Ndipo unahusika kuhusu ndugu yako, kama Roho yumo ndani ya Kristo.

¹³³ Kwamba, Yeye alihusika sana, hata akatoka Mbinguni, akaiacha Mbingu, akashuka humu duniani, na kuzaliwa katika zizi la samadi pamoja na kundi la ng’ombe wanaolia, bila hata na nguo za kumvalisha. Yeye—Yeye alishiriki. Hana mahali pa kulaza kichwa Chake; hana kaburi la kuzikiwa; alipigwa na kuchubuliwa, jinsi alivyokuwa. Alihusika vya kutosha, na Mungu aliupenda ulimwengu sana, hata akamtoa Mwanawe wa pekee.

¹³⁴ Na mambo hayo yote pale, kwamba huyo Roho aliyekuwa ndani Yake yuko ndani yako, halafu sisi hatuhusiki mmoja kwa mwingine na kuhusu kanisa?

¹³⁵ Watu wananiambia, wakati wote. Mtu fulani alisema, si muda mrefu uliopita, alisema, “Ndugu Branham, acha kulikemea kanisa. Acha kusema mambo haya. Hayo si juu yako kuyasema.”

Nikasema, “Ni nani atakayeyasema basi?” Unaona? Hiyo ni kweli.

¹³⁶ Hilo, hakika, ni—ni jukumu letu. Ni jukumu letu, watu kuwaambia Ukweli kabisa, maana utakutana nalo tena. Haya ni makao ya muda tu; yale ni ya Milele kule. Na tudumu nalo, tuseme ukweli na tuwe waaminifu juu ya jambo hilo. Naam, kuhusika.

¹³⁷ Kwanza, kabla hujahusika, huna budi kushawishika uko sawa. Ndipo wakati umeshawishika ya kwamba Mungu ni wa kweli, na Mungu yumo ndani yako, na Mungu alifanya mambo makuu namna hiyo kwa ajili yako, basi una hakika. Ukimwona ndugu yako makosani, utamwambia kuhusu jambo hilo. Kama hakuna, kuna kasoro fulani. Hiyo ni kweli, sasa.

¹³⁸ Na kama ukiona kwamba kanisa limekosea. Wewe, haidhuru, unalipenda kanisa. Na—na unaninii... Kristo alilipenda Kanisa na akautoa uhai Wake kwa ajili Yake. Nasi tunapaswa kufanya jambo lile lile. Si kwamba tu tunapaswa kufanya, bali tutafanya hivyo kama tuna upendo wa Kristo ndani yetu. Inatubidi na inatupasa kufanya hivyo, kama Wakristo. Naam.

¹³⁹ Mara Andrea aliposhawishika ya kwamba huyo alikuwa ni Masihi, yeye alifanya nini? Hapana shaka usiku huo, akiketi pale mkutanoni, ambapo yeye na—na mwenziwe. Kristo aliketi nyumbani pale, hapana shaka ila Yesu alirudi moja kwa moja katika Maandiko na kuanza kumwambia.

¹⁴⁰ Sasa, Andrea alikuwa mwanachuoni, kwa maana baba yake alikuwa mwanachuoni. Yeye, yeye na Petro, walikuwa. Baba yake alikuwa Mfarisayo, naye alikuwa mtu mzuri, aliyefunzwa. Na kwa hiyo alijua vile Masihi angekuwa.

¹⁴¹ Ndipo wakati alipomwona Masihi akifanya mambo ambayo Masihi anapaswa kufanya, alipoona jinsi Yeye alivyoishi na kila kitu, alishawishika ya kwamba huyo alikuwa ni Masihi.

¹⁴² Sasa, unapomwona Mungu amekushika, na kuyabadilisha maisha yako, kukufanya kutokana na jinsi u—u... vile usivyo, kufikia vile unavyopaswa kuwa, basi wewe uko tayari kumwambia mtu mwingine kuhusu jambo hilo. Umeshawishika.

¹⁴³ Lakini shida yake ni kwamba, tunaenda huku, tuna njia fupi, nyepesi ya mkato. Tunaninii tu, “Loo, hatuwezi kukaa pale muda mrefu wa kutosha. La, usizungumze nasi kwa muda wa siku kumi, ama usiku kucha.” La, inatupasa kwenda kule, na labda tutapeana mikono na mhudumu, ama kuandika jina letu kwenye kitabu, ama kupitia katika mhemuko mdogo. “Tumempata.”

Nje, usiku, usiku mmoja kwenye baa, usiku unaofuata kuhubiri Injili. Unaona? Unaona? Loo, jamani! Hapo ndipo, ndipo palipo na shida. Hiyo ndiyo sababu tunachanganyikiwa sana kuhusu, unaona, juu ya mambo hayo. Mtu na ajithibitishe.

¹⁴⁴ Ninakumbuka mahubiri ya kwanza niliyojaribu kuhubiri. Ninamthamini maskini yule mhubiri mzee wa Kibaptisti. Nilisimama pale. Nami niliona jinsi alivyohubiri. Nilikuwa tu mvulana mdogo, nilikuwa kwenye Njia yapata miezi sita ama mwaka mmoja. Naye akaniita kule, kasema, “Sasa ninataka uhubiri kesho, ama Jumatano usiku.”

¹⁴⁵ Nikasimama mimbarani. Nilidhani nilifanya tu kama mhubiri. Nilidhani nilifanya vizuri. Akina mama wazee, baadaye, walinipigapiga mgongoni na kusema, “Ndugu Billy, huo ulikuwa tu mzuri sana!” Mama wazee, mwajua, hapo karibu, wakilia, kasema, “Na Mungu atakufanya mhubiri.”

Nikawazia, “Loo, natumaini atanifanya.” Nilidhani nilifanya vizuri sana.

¹⁴⁶ Nilienda huko kwa Dkt. Davis, akiwa ameketi pale, mdomo wake ukining’inia chini. Nikasema, “Nilifanyaje, daktari?”

Kasema, “Mabaya sana niliyopata kusikia.” Unaona?

¹⁴⁷ Nikawazia, “Loo, jamani!” Nilifikiri nilipitia kwenye mihemuko yote na kila kitu nilichopaswa kufanya, kurusharusha mikono yako na chochote kile, wajua, kama mhubiri anavyofanya. Nilifikiri nilikuwa nimefanya kila moja ya hayo. Nilikuwa nimemwangalia na kufanya vile hasa alivyofanya.

Akasema, “Mabaya sana niliyopata kusikia.”

Nikasema, “Ati nini Ndugu Davis?”

¹⁴⁸ Akasema, “Sijawahi kusikia kama hayo maishani mwangu.” Akasema, “Kijana, ninataka ukutane na mimi kwenye chumba changu cha kusomea, kesho alasiri, saa nane.”

¹⁴⁹ Nikawazia, “Loo, jamani!” Kwa hiyo saa nane nilishuka nikaenda kule, huku manyoya yangu yote yameng’olewa, wajua. Nikasema, “Habari za jioni, Dkt. Davis.”

Kasema, “U hali gani, Billy? Ketu chini.”

Nikasema, “Naam, bwana.”

Akasema, “Nadhani hisia zako zimeumizwa.”

¹⁵⁰ Nikasema, “Zimekanyagwa tu. Hivyo tu.” Nikasema, “Vema, nini, nilikosea wapi?”

¹⁵¹ Akasema, “Ninataka kukwambia hadithi ndogo.” Kasema, “Unajua, nilisoma, nilikuwa wakili kabla sijakuwa mhudumu.”

Nikasema, “Naam, bwana. Ninajua jambo hilo.”

152 Akasema, “Billy, wakati mmoja nilisoma sheria, nami nilisoma jinsi tu ulivyoisoma Biblia, ama jinsi ulivyojifunza kuhusu huduma.”

153 Akasema, “Nilifikiri ya kwamba nilikuwa wakili nilipoapishwa mahakamani.” Akasema, “Nilienda kule na kutetea kesi fulani ya talaka wakati mmoja, kesi yangu ya kwanza.” Kisha akasema, “Nilikuwa nimewaona hao mawakili wakipigapiga meza namna hiyo, na kupaza sauti ‘Mheshimiwa, bwana, Hakimu!’ Na kulia na kupanguza uso wao, kwa machozi. ‘Maskini mwanamke huyu, yeye ni *fulani*,’ na jinsi hiyo.” Kasema, “Na baada ya kitambo kidogo, yule wakili mzee, aliyekuwa mpinzani wangu, upande wa pili,” kasema, “aliketika tu pale na kuniangalia kwa muda mrefu.” Kasema, “Nililia. Nikagongagonga meza, na kufanya kila kitu kama mawakili walivyofanya.” Kisha kasema, “Jamani! Mzee mpinzani wangu aliketika pale, hao mawakili wangine upande huo mwingine, wakili wa mtu huyo aliketika pale. Mara akasema, ‘Hakimu, Mheshimiwa, hii mahakama yako inaweza kuvumilia kiasi gani zaidi cha upuuzi huu?’”

154 Kasema, “Nilipoteza kesi hiyo.” Kisha kasema, “Nilishindwa kwelikweli.” Akasema, “Nilijifunza jambo fulani wakati huo, unaona. Yeye... Nami nikamwuliza hakimu. Akasema, si... Kasema, “Wakili huyo, pia, alikuwa ni rafiki yangu. Lakini,” kasema, “alishuka akaja pale, na kusema, ‘Roy, nilifanya hilo maksudi.’ Kasema, ‘Unaona, ulikuwa na mihemuko. Ulikuwa ukilia, ukitikisa kichwa chako, na kukipigapiga.’

“Kasema, ‘Ninafanya tu kama mawakili wengine wanavyofanya.’

155 “Akasema, ‘Lakini hukuwa ukiweka hata chembe moja ya sheria ndani yake. Si mihemuko yako inayoshinda kesi; ni uamuzi wa sheria. Inakubidi kujua vile sheria inavyosema juu ya jambo hilo.’”

156 “Na hilo ni jambo lile lile leo, kukuhusu wewe.” Kasema, “Billy, ulikitikisa kichwa chako, na ukalia na kurukaruka, bali kamwe hukuhubiri neno moja kutoka katika Biblia. Ulipitia katika mhemko wa kila namna.”

157 Neno la Mungu ndilo muhimu. Neno la Mungu ndilo linalosema. Kweli kabisa. Haina budi kuwa ni Neno, Neno halisi.

158 Na ndipo walipoliona Neno hilo limefanyika mwili katika Yesu Kristo, Andrea alishawishika kabisa, na ndipo akahusika juu ya ndugu yake. Akaenda upesi sana.

159 Je! Uliona? Kamwe yeye hakusema, “Njoo huku, Simoni. Ni—ni—ninataka uje huku na uketi mkutanoni pamoja nami. Labda huenda ikawa tungeweza kutambua roho, na tungeweza kujua kama Mtu huyu kweli ni Masihi au siye.” Hakusema hivyo kamwe.

¹⁶⁰ Akasema, “Tumempata.” Hakukuwa na kugugumiza juu ya jambo hilo. “Tulimpata Masihi. Njoo, mwone.” Alikuwa ameshawishika kabisa.

¹⁶¹ Musa, vivyo hivyo, wakati alipowazia kuchukua mamlaka, huko Misri, na akamwua Mmisri, hakuwa amehusika. Hakuninii... Hakuhusika juu ya jambo hilo. Kama Mungu alikuwa awe pamoja naye, mbona hakuwa pamoja naye?

¹⁶² Kwa hiyo alitoka akaenda akamwoa mwanamke mrembo. Na kwa hiyo alipata mtoto kwake, Gershomu, na—nao walitulia. Naye alikuwa atarithi kundi kubwa la kondoo huko nje kutoka kwa Yethro, yule kuhani M—Mmidiani. Naye alikuwa, kila kitu, kilikuwa rahisi. Angeishi pamoja na mke wake, na kuwa na makazi madogo, na, mwajua. Ninii tu, alikuwa akiishi vyema; kazi nzuri, alikuwa awe mrithi. Kila kitu kilikuwa sawa.

¹⁶³ Hakuhusika. Hakuhisi kiboko cha msimamizi tena. Ha—hakuhusika juu ya ndugu zake kule chini: kuhusu wakunga wabaya; na—na hao wanawake wakizaa watoto wao, waliokuwa wamewapasua vichwa vyao na kuwatupia mamba; na—na, wao, jinsi walivyokuwa wamewafanya watumike sana kule chini; na—na katika utumwa na kifungo. Yeye hakuvutiwa.

¹⁶⁴ Alikuwa amelipia makazi yake, kama tu vile tunavyofanya siku hizi. Hilo ndilo jambo la kwanza tunalofikiria: kulipia nyumba. Hilo ni sawa. Unapaswa kufanya hivyo. Hiyo ni kweli. Lakini kuna kitu kinachopaswa kutukia kabla ya jambo hilo.

¹⁶⁵ Ni Mungu, kwanza, mambo yanayoendelea kanisani. Ni wajibu wa kila mtu katika kanisa hili papa hapa, kuona ya kwamba kila kitu jambo hilo linaenda sawa. Nawe unaweka nguvu zako kwake, kumleta kila mwanamume na mwanamke, mvulana kwa msichana, uwezaye, njiani, mipakani, na barabarani, kumleta kanisani.

¹⁶⁶ Musa alikuwa ameketi kitako. “Waache. Nadhani, kama hivyo ndivyo wanavyotaka kufanya jambo hilo, sawa.” Unaona? Yeye hakuwa amewahi kupata ujuzi wa kibinafsi bado.

¹⁶⁷ Kwa hiyo, siku moja, huko upande wa nyuma wa jangwa, kulikuwako na mchungaji mzee mwenye mandevu aliyeshuka pale kilimani, akiwa na fimbo mkononi mwake. Aliingia, uso kwa uso na Mungu; Yehova Mungu ameketi juu kule kichakani, nacho kikiwaka moto. Mungu aliuvutia usikivu wake vya kutosha kumpeleka pale na kutoa viatu vyake. Naye akaisikia Sauti ya Mungu. Alishawishika, ya kwamba “MIMI NIKO AMBAYE NIKO. Sishindwi kamwe. Mimi Ndimi niliyekuwa pamoja na Ibrahimu, Isaka, na Yakobo. Mimi ningali Mungu yule yule.” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁶⁸ Ndipo wakati alipoona ya kwamba Mungu hakuwa tita la kanuni za imani, Mungu hakuwa tita la mafundisho; Mungu alikuwa halisi, hai, aliye hai, moyo wake uliwaka moto. Hakuna kitu kitakachomkomesha sasa. Naye alikuta kwamba kusudi la

Mungu lilikuwa ni kuwakomboa Israeli, naye alikuwa ameitwa kwa ajili ya kazi hiyo.

¹⁶⁹ Ee Mungu, tupe wahubiri kama hao. Hivyo ndivyo sisi... Hicho ndicho tunachohitaji, ndugu. Sivyo, ndugu? [Ndugu wanasema, “Amina.”—Mh.] Hiyo ni kweli. Badala ya kukimbilia mahali pengine.

¹⁷⁰ Ujuzi wote wa Musa wa seminari ulikwisha wakati huo. Unaona? Yeye—yeye alikuwa mtu mwerevu. Alikuwa amefunzwa katika hekima yote ya Wamisri; angeweza kuwafundisha. Lakini haikufaa kitu. Ilimpasa kuwa na ujuzi wa kibinafsi na Mungu. Naye alikutana Naye pale, uso kwa uso, naye akanena Naye. Na mara aliponena Naye, alijua wazo lake lilikuwa ni nini, na mpango wake ulikuwa nini, alihusika papo hapo juu ya ndugu zake waliokuwa utumwani.

¹⁷¹ Na mwanamume yeyote ama mwanamke anayekutana na Mungu kamwe, uso kwa uso, naye anaweza kuondoka na kulichukulia kama jambo rahisi, kuona watu mitaani, wakigaagaa katika dhambi, linakuua.

¹⁷² Nilimwambia mke wangu, wakati fulani uliopita, na baadhi ya ndugu zangu. Nilisema, “Je! nimeingiwa na kichaa? Mimi ni mwendawazimu? Kwa nini ninaendelea kuwakemea watu? Kwa nini ninasema jambo hili? Nami ninafunga,” nikasema, “ninafunga na kuomba, kuondokea jambo hilo.” Kadiri ninavyofunga, ndivyo dhambi inavyozidi kuwa mbaya zaidi. Unaona? Linaifanya tu kuwa mbaya zaidi, mpaka, kwa kweli, hata huwezi kutoka nje.

¹⁷³ Mke wangu alitaka kwenda nami kwenye namna fulani ya duka, hivi majuzi. Nikaenda mlangoni, na huyu hapa bibi mmoja anakuja kupitia pale. Nami ninajua mahali mwanamke huyu anakoenda kanisani. Na, yeye, lilikuwa ni jambo baya sana. Nikasema kwa sauti kubwa, “Rudi, ewe zimwi. Nitakuwa mzuri.” Niliona hizo nywele kubwa, zilizotuna namna *hiyo*, kukiwako na rangi ya kijanikibichi iliyoonekana bluu *huku*, na chini *hivyo*. Alikuwa akiyumbayumba kupitia pale, alionekana kama mnyama aliyechinjwa, akakazwa, huko nje katika nguo hizo. Ninawaambia, loo, lilikuwa jambo baya sana. Kweli.

¹⁷⁴ Nilikuwa kwenye kiamshakinywa cha Wafanyabiashara hivi majuzi, huko Los Angeles, nami nilikuwa nimesimama pale nikiimngojea Ndugu Arganbright angie. Ndipo bibi mmoja akaingia ndani. Sijapata kuona kitu kama hicho. Nikawazia, “Loo, jamani, angalia maskini kitu kile! Yeye, ana kasoro fulani.” Kwa hiyo nikaanza, ni—nikaanza kuondoka.

¹⁷⁵ Nikasema, “La. Mimi ni mhudumu. Ninapaswa kuzungumza naye. Ni—nimeona nimeona kansa. Nimeona ukoma. Sijawahi kuona kitu kama hicho. Yeye ni kijanikibichi kote chini ya macho yake.” Nikaanza. Nikaenda pale. Sasa, wanadamu

hawaonekani hivyo, isipokuwa wawe wamekufa ama kitu fulani, ama wameoza. Kwa hiyo, nikaenda pale.

¹⁷⁶ Nami nikawazia, mwajua, nilikuwa nimwendee na kusema, “Dada, samahani. Mimi—mimi ni muhudumu, na huduma yangu ni kuwaombea wagonjwa. Sijui, bali je! ungetaka nikuombea?”

¹⁷⁷ Na wakati nilipokuwa nikiwazia, huyu hapa mwingine anakuja, na mwingine anakuja. Ndiyo mara ya kwanza nilipokuwa nimeona kitu hicho, rangi isiyo ya kawaida kabisa *huku*, wajua, na—na—na bluu *hapa* juu, na kijanikibichi *hapa* chini. Na ilikuwa ni tamasha ya kigeni sana. Na, kusema kweli, kichwa kikubwa *hivi*. Si—sijapata kuona kitu chochote kama hicho. Nilisikia aibu sana.

¹⁷⁸ Mbona, ni fedheha! Hakika ndivyo. Na amevaa nguo ndogo, kama, wajua, suruali, wanavyoziita. Wakati, Biblia ilisema, “Mwanamke anayevaa mavazi yampasayo mwanamume, ni chukizo mbele za Mungu.” Loo, kitu hicho chote hakina budi kuwa ni harufu mbaya mbele za Mungu. Na moyo wako unawezaje kuangalia jambo hilo, wala usihusike? Wakati, unaona taifa lako mwenyewe, watu wako mwenyewe, wanadamu wakitetemeka katika mateso, wakielekea jehanamu, wala huwezi kufanya jambo lolote kuhusu hilo. Hebu nipige makelele mradi ningali na sauti ya kupiga makelele. Sijali yale mtu yeyote asemayo. Kuna mema na mabaya. Ninataka upande ufaao wakati nitakaposimama mbele za Mungu. Ninataka kusimama. Naam. Hakika.

¹⁷⁹ Musa alihusika wakati alipoona kwamba Mungu alikuwa ni Mungu. Alihusika.

¹⁸⁰ Yakobo, usiku mmoja, mwajua, alikuwa amemwacha Labani, naye alikuwa akienda zake kule. Shauku iliingia moyoni mwake kutembelea nchi ya uenyeji wake. Nasi sasa tunaona ya kwamba alihofu. Hakuwa . . . Alihofu kukutana na ndugu yake. Kwa hiyo akaanza kushughulika, kabla ya kuvuka Yordani, naye akaomba usiku kucha. Ndipo akashindana mwereka na Bwana, akashindana mwereka usiku kucha. Loo, akasema, “Sitakuacha uende.”

¹⁸¹ Ninapenda jambo hilo. Mshikilie. Kweli. Kaa usiku kucha pamoja Naye. Andrea alifanya hivyo. Alikaa usiku kucha pamoja Naye.

¹⁸² Naye akashindana mwereka na Malaika, usiku kucha. Ndipo huyo Malaika akasema, “Kunapambazuka. Sina budi kuondoka.”

¹⁸³ Akasema, “Sitakuacha uende kamwe. Ninataka kitu fulani ndani yangu ambacho ni tofauti. Ninataka kitu ndani yangu kitakachonibadilisha.”

¹⁸⁴ Nanyi unaona, mara Bwana alipombariki, baraka aliyoomba, alikuwa tayari basi kuvuka mto na kwenda

kumwona ndugu yake. Unaona? Kwa nini? Alikuwa ameshindana mwereka usiku kucha. Alikaa pamoja na—alika pamoja na . . . pamoja na Mungu, usiku kucha, na kushindana mwereka na Mungu.

¹⁸⁵ Sasa, kama alisema tu, “Aisee, niache sasa. Nimechoka.” Unaona? Hiyo baraka kamwe isingelikuja. Unaona? Yeye kamwe—kamwe asingekuwa hapo. Unaona?

¹⁸⁶ Lakini alikaa usiku kucha. Unaona? Alishindana Naye mwereka usiku kucha, ndipo akawa tayari kwenda kukutana na ndugu yake kesho yake asubuhi.

Maskini Daudi, wakati mmoja . . .

¹⁸⁷ Unaona, jambo la kwanza, huna budi kushawishika. Halafu, jambo la pili, unahusika baada ya kushawishika. Sasa, Yakobo alijua. (Kabla sijamwendea Daudi.) Yakobo alijua ya kwamba Mungu aliyekuwa amemtenga na ndugu yake, Mungu aliyekuwa amemtuma katika nchi nyingine na alikuwa pamoja naye, na kumbariki na kumpa yote aliyokuwa nayo; na alikuwa amempa ahadi, ya kwamba angemtunza, kumzidishia, kama angerudi kwenye nchi yake. Yeye alijua, kama angeweza tu kuwasiliana na Mungu huyo, basi angehusika, kwa hiyo akafanya hivyo. Vema.

¹⁸⁸ Sasa, Daudi, siku moja alikuja kuleta keki cha—chache za tini, na baadhi ya pai za zabibu kavu ambazo baba yake alikuwa ametayarisha. Yese alikuwa amemtuma Daudi. Alikuwa ni mvulana mdogo, na ndugu zake walikuwa huko vitani pamoja na Waisraeli. Nao Wafilisti walikuwa wamewasukuma, na walikuwa wamewasukumia kando ya kilima, nao Wafilisti walikuwa upande huo mwingine. Ndipo maskini Daudi akaja amevaa koti lake dogo la kichungaji, kombeo limekunjwa na kuwekwa mfukoni mwake ama popote pale. Ba—basi akapanda kwenda kule, ndipo akasikia m—mngurumo mkubwa ukitoka kwenye jitu moja kule juu, likiyapa changamoto majeshi ya Mungu aliye hai.

¹⁸⁹ Vema, hilo kwa namna fulani lilimkasirisha Daudi sana. Unaona? Sasa, Daudi alimwendea Sauli, naye akamwambia Sauli. Baada ya habari hiyo kuenea, yale aliyosema, angeenda kupigana naye. Alienda kwa Sauli. Naye Sauli akasema, “Vema, wewe si kitu ila mvulana. Nawe ni maskini mvulana mdogo mwekundu. Naye ni mkubwa mara nyingi kwa kimo chako, amekuwa shujaa tangu ujana wake. Ungewezaje kamwe kupigana na mtu kama huyo?”

¹⁹⁰ Sasa angalia. Daudi, kwanza, alishawishika. Amina. Alishawishika, ndipo akahusika juu ya ndugu zake. Kama walihofu sana kupigana naye, yeye angepigana naye. Amina.

¹⁹¹ Haya basi. Ni Mkristo wa aina hiyo. Kama hao wengine hawatafanya jambo hilo, hebu tulifanye. Amina. Hebu. Kama itanibidi kusimama peke yangu, na kusimama pale. Paza sauti, mema na mabaya. Litangaze huko nje. Litangaze, haidhuru

mtu yeyote anasema nini kukuhusu wewe. Simama na Neno la Mungu na useme ni la kweli. Dumu Nalo. Loo, ni wakati wa jinsi gani!

Daudi alishawishika. Alijua Mungu alikuwa halisi.

¹⁹² Kwa hiyo huenda Sauli alisema kitu kama hiki, “Mwanangu, ninavutiwa na ujasiri wako. Lakini, wewe, humwezi mtu huyo.” Unaona, walikuwa wakimwalia kwa nje.

¹⁹³ Lakini Daudi alikuwa ameshawishika. Akasema, “Sikiliza. Siku moja,” akasema, “mtumishi wako hapa alikuwa akiwachunga kondoo wa baba yake.” Kisha kasema, “Simba alikuja, na kumshika mmoja wa hao wana-kondoo, akatoroka naye.” Ndipo akasema, “Mtumishi wako alimfukuza, nami nikamwangusha chini, kwa kombeo. Sasa yeye alinirukia, nami nikamshika ndevu nikamwua.”

¹⁹⁴ Akasema, “Ndipo siku moja mnyama mwingine, dubu, alikuja na kumshika mmoja, akakimbia. Nami ni—nikamwua. Nimeshawishika ya kwamba Mungu ambaye angeweza kuniokoa na makucha ya simba, kutoka kwenye makucha ya dubu, ni zaidi sana jinsi gani Yeye ataniokoa na Mfilisti huyo asiyetahiriwa, anayejigamba kule?” Naam, bwana. “Ni zaidi sana jinsi gani atafanya hivyo? Nimeshawishika kwamba ni kweli. Nao ndugu zangu hawana ujasiri wa kupigana. Hiyo ni kweli. Lakini nimeshawishika kuhusu majeshi ya Mungu aliye hai. Ninahusika, kuwaona wakirudi nyuma kwenye masuala haya.” Amina.

¹⁹⁵ Je! nilisema jambo fulani? Vema. Naam, bwana. Ninahusika ya kwamba wamerudi nyuma juu ya suala la Mungu, wakisema, ya kwamba, “Yesu Kristo si yeye yule jana, leo, na hata milele.” Ninahusika kuhusu wao kurudi nyuma, na kusema, “Utakatifu si mali ya kanisa. Hakuna kitu kama kutakaswa kwa Roho.” Ninahusika kuhusu wao kusema, “Siku za miujiza zimepita.” Shida yao ni ipi? Kuna nini? Sisi tunahusika.

¹⁹⁶ Kama wanahofu kufanya jambo hilo, tumekuwa na ujuzi kule. Tulikutana na Ibilisi. Hiyo ni kweli. Na Mungu ambaye angeweza kumshinda Ibilisi maishani mwangu, na kunimwagia ubatizo wa Roho Mtakatifu, anaweza—anaweza kumwua yule ibilisi asiyetahiriwa huko nje, ambaye anajaribu kuyatukana majeshi ya Mungu aliye hai. Amina.

¹⁹⁷ Daudi alikuwa amehusika. Kwa nini? Alikuwa ameshawishika ya kwamba Mungu ni Mungu. Alikuwa ameshawishika ya kwamba Mungu ambaye angeweza kumchukua yeye pamoja na kombeo hilo na kumwua simba, angeweza pia kumdhibiti Mfilisti huyo mwenye majivuno, asiyetahiriwa. Hivi huwezi kuona jambo hilo, ewe rafiki?

¹⁹⁸ Mungu ambaye anaweza kumjaza mtu na Roho Mtakatifu, hivi hawezi kumponya mwanamume ama mwanamke, anayejaribu kumkaidi Mkristo? Loo, hakika anaweza. Moyo

wenye njaa unaotaka kumjua Mungu, Mungu ambaye alimshinda Ibilisi na kumtoa maishani mwangu, na kumweka Kristo mle ndani, hivi Yeye hawezi kufanya jambo hilo kwa ajili ya mtu huyo pia? Hakika. Mungu ambaye anaweza kukuondolea shauku za ulimwengu, hivi hawezi kuondoa tamaa za ulimwengu kutoka kwa mtu huyo mwingine? Hakika, Yeye anaweza. Unaona, jambo ni kwamba, inakubidi ushawishike, na ndipo unaweza kuhusika baada kufanya jambo hilo.

¹⁹⁹ Katika Waamuzi tunamwona mwamuzi wa tatu. Wengi wenu kamwe hamjaisoma. Jina Lake lilikuwa Shamgari. Kifungu kimoja, kidogo, ndicho kimeandikwa juu yake, chini ya kurasa za—za Biblia, katika Biblia yangu ya Scofield hapa. Naye shamgari, yeye alikuwa ni Mwi—Mwisraeli.

²⁰⁰ Na wakati wa Waamuzi, Wafilisti walikuwa wamewaacha Waisraeli wote wakuze mimea yao. Nao wangepanya nini? Wangukuja huko, waingie, baada ya wao kufanya kazi katika msimu wote wa kiangazi, wawanyang'anye mimea yao, warudi moja kwa moja.

²⁰¹ Siku moja, maskini Shamgari huko nje, alikuwa amesimama, alikuwa na ghala lake, akamaliza kabisa kupura, alikuwa ameweka ngano yake. Na labda maskini mke wake, kwa namna fulani mgumu, watoto wake wachanga, wajua, wenye mashavu yaliyokwanjuka. Iliwabidi kuishi kwa shida sana, kwa sababu, mwaka uliopita, Wafilisti walichukua kila kitu. Iliwabidi tu kuokotaokota kote, wapate walichoweza kupata. Na ndio hao hapo katika hali hiyo.

²⁰² Na mnamo wakati Shamgari alipoweka kila kitu tayari kwa ajili ya kipupwe, alisikia kelele. Akaangalia nje ya dirisha. Ni kitu gani kilichokuwa kikija? Hawa hapa Wafilisti mia sita wanakuja, wote wana silaha: mikuki, mapanga yakining'inia mbavuni mwao, dirii zenye kina cha inchi moja hivi, za shaba; kubwa mno, wamefunikwa namna hii, kwa chuma, na dereya za chuma, kama wanavyoiita. Hawa hapa. "Pump, pump, pump." Vema, wakapanda moja kwa moja kwa utaratibu. Ati nini? Kuchukua kile alichokuwa nacho. Jambo ndilo hilo. Unajua nini? Shamgari, ningeweza tu kuwazia, aligeuka na kuiangalia familia yake. Akaangalia huko nje kwenye wale Wafilisti.

²⁰³ Kisha akaangalia Mbinguni. Akawazia, "Mimi ni Myahudi. Niko katika Agano. Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na Yakobo, baba yangu, ni Mungu wangu. Mimi nimetahiriwa. Mimi si mpiganaji. Sijui kitu kuhusu upanga. Lakini ninahusika juu ya familia yangu. Nimeshawishika ya kwamba Wewe ni Mungu." Haleluiya! Jambo ndilo hilo.

²⁰⁴ Sio kupiga makelele, "We, Bw. Mfilisti, ngoja mpaka nitakapopata Digrii yangu ya Sanaa, wajua, Ph. D. yangu. Nitajifunza jinsi ya kupigana kwa mapanga." La. Huna wakati wa jambo hilo. Jua tu ya kwamba Yeye ni Mungu. Hivyo tu.

205 Akasema, “Ninajua ya kwamba Yeye ni Mungu. Nimeshawishika ya kwamba Yeye ni Mungu. Ninajua ya kwamba mimi ni Myahudi. Ninajua ya kwamba niko katika lile agano. Ninajua ya kwamba nimetahiriwa.” Loo jamani!

206 Siku hizi tunatahiriwa kwa tohara kubwa kuliko hiyo. Tunatahiriwa kwa Roho Mtakatifu, wakati ulimwengu wote unakatiliwa mbali kutoka kwako. Je! uko katika agano? Wewe ni Mkristo? Je! umejazwa na Roho Mtakatifu? Umetahiriwa na Roho Mtakatifu? Basi, ndugu, kila ahadi katika Biblia ni yako. Amina.

207 Mungu ana neema hapo kuwafanya ninyi wanawake mzifanye nywele zenu ziwe ndefu. Ana neema mle ndani kuwafanya ninyi wanaume mwone kwamba anazifanya ndefu. Ana neema humo ndani kwa ajili ya mambo haya yote. Ana neema humo ndani kwa ajili ya uponyaji wenu. Kweli. Yeye ni Mungu.

208 Kama sivyo, tunachezea nini, tunapiga makelele ya nini? Sisi ni shaba iliayo na upatu uvumao, na tumekuwa “chumvi iliyopoteza ladha yake.” Kweli.

209 Sisi ni wapentekoste, ama sivyo? Jambo lingine, kama sisi ni wapentekoste, hebu na tuwe wapentekoste. Kama Ujumbe ni wa kweli, ingia ndani Yake. Kama si wa kweli, toka ndani Yake ukatafute mahali pazuri. Hakika. Kama Mungu ni Mungu, mtumikie. “Bali huwezi kumtumikia Mungu pamoja na mali wakati ule ule.” Hebu na tumtumikie Mungu. Shawishikeni, ndipo basi mtahusika. Ndipo kanisa kweli litaanza kukua, maana mtatoka nje na kumleta kila mtu mwezaye na kumwingiza ndani.

210 Lakini mradi tu unazungukazunguka, kusema, “Vema, hiyo ni kazi ya mhubiri.” Sio kazi ya mhubiri. Ni kazi ya kila mtu. Kweli. Kila Mkristo aliyezaliwa mara ya pili ana Roho yuyo huyo ndani yao. Huenda mhubiri ana kipaji, bali hiyo ni karama tu ya Roho Mtakatifu, si Roho Mtakatifu; karama ya Roho Mtakatifu.

211 Wahubiri huitwa. Manabii, na waalimu, na wainjilisti, na wachungaji, na kadhalika, wanampokea Roho Mtakatifu, halafu karama ya kufanyia mambo haya.

212 Lakini Mungu hana watoto wowote wadogo sana ama watoto wakubwa mno. Wote ni watoto, Kwake. Hiyo ni kweli kabisa. Na mahali pako panapofaa ni kuketi sasa hivi katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, pamoja na kila nguvu.

213 Unasema, “Ndugu Branham, mimi ndiye mdogo sana kanisani. Mimi ni kajamaa kadogo tu.”

214 Lakini, kumbuka, alipopaa Juu, unaona, ulipaa pamoja Naye. Wewe uko katika ule Mwili. Nawe uko pamoja na Kristo sasa hivi, umeketi katika ulimwengu wa Roho. Kama wewe ni ngozi iliyo chini ya miguu, kila pepo yuko chini yako. Hiyo

ni kweli. Kweli kabisa. Kanisa! Palipo na kichwa, mwili upo pamoja nacho. Na kama tumezikwa, tumekufa, kuzikwa katika Kristo, basi tumefufuliwa pamoja Naye katika ufufuo Wake, na tunaketi katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, na kila moto wa kuzimu ukiwa chini yetu. Amina. Kweli. Haidhuru wewe ni mdogo jinsi gani, kila pepo yuko chini yako. Kwa nini? Mshindi wetu mkuu ameshinda kila dhambi, kila kitu, kila ugonjwa, kila . . . hata mauti yenyewe. Hiyo ni kweli. Sisi ni zaidi ya washindi katika Yeye. Jambo pekee, tumeketi pamoja Naye katika Kiti Chake cha Enzi, tukimwangalia wakati Yeye akiangalia huko, Baba. Jambo ndilo hilo. Liko hapo. Vema.

²¹⁵ Shamgari alichoshwa na jambo hilo. Akasema, “Nimeshawishika kwamba Yeye ni Mungu. Ninahusika pamoja na familia yangu.” Unajua alichofanya? Alichukua konzo hilo la ng’ombe, akaruka pale katikati ya barabara, akawaua Wafilisti mia sita.

²¹⁶ Unajua mchokoro wa ng’ombe ni kitu gani? Mbona, ni fimbo, yenye urefu wa, loo, nakisia, kama futi sita, saba, labda si ndefu hivyo, pamoja na kipande kidogo cha shaba kwenye ncha yake, ama chochote kile, ama chuma. Na wakati plau inapokwama, wakati mwingine wanaichakura plau kwayo, namna *hiyo*, kisha wanampiga maksai nayo, namna *hiyo*, “Haraka! Haraka! Ruka twende.”

²¹⁷ Namna *hiyo*, akiwa na fimbo mkononi mwake. Na, yeye, akiwa hana kitu ila ovaroli zake tu. Zilikuwa ni nguo za kulimia. Na hapa hawa Wafilisti walikuwa wamevaa chepeo na silaha, pamoja na mkuki. Na maskini Myahudi huyo mmoja, hakuwashinda kabisa tu, bali aliwaua. Amina. Fimbo *hiyo* ilistahimilije? Pigo la kwanza alilopiga kichwa cha mfilisti aliyevaa silaha, nene *hivyo*, konzo hilo la ng’ombe lilipasuka vipande hamsini. Lakini aligonga mmoja upande mmoja, na mwingine huo mwingine, namna *hiyo*, mpaka akalibwaga chini kundi lao zima na kuwaua. Kwa nini? Kwa sababu alikuwa ameshawishika. Amina. Alihusika.

²¹⁸ Kama mwanamume angepigania familia yake namna *hiyo*, chini ya hali ya mambo kama hayo, je! Kanisa la Mungu aliye hai linapaswa kupigana na kitu gani, kwa ubatizo? Shamgari alikuwa na konzo la ng’ombe. Wewe una ubatizo, Roho Mtakatifu. Loo, jamani!

²¹⁹ Hatutaki saa nne usiku wa leo, kwa *hiyo* inatupasa kuendelea. Vema. Naam, bwana.

²²⁰ Ibrahimu, unajua alichofanya? Alikaribisha, siku moja. Ninasahau, ni moja kwa moja karibu mlango wa 16, 17, la, karibu wa 19, nadhani, wa Mwanzo. Aliwakaribisha, siku moja, kundi la Watu, mpaka aliposhawishika kabisa kwamba walikuwa ni akina Nani. Aliinua macho yake wakati alipokuwa ameketi huko

nje chini ya hema. Aliona Watu watatu wakija; nguo zilizoja mavumbi. Akawaangalia. Yeye alikuwa . . .

²²¹ Hisia ndogo za kigeni zilimjia, ya kwamba hao Watu walikuwa kidogo wako tofauti na watu wengine, kwa hiyo akakimbia kuwalaki. Akasema, “Hivi mbona msije, mkaketi chini chini ya mwaloni, na,” kasema, “na mpumzike kidogo? Nami nitawatafutia maji kidogo. Na nitaitawadha miguu Yenu. Na—na nitawapa kipande cha mkate. Kisha mjiburudishe, ndipo mwaweza kuendelea na safari Yenu.” Unaona?

²²² Ilikuwa ni kitu gani? Yeye asingeachilia nafasi hiyo ipite. Usifanye hivyo usiku wa leo, pia. Unaona? Alikuwa anakwenda kushika nafasi hiyo.

²²³ Sasa, alisema, “Wewe keti papa hapa sasa, nami nitaingia ndani na kukuletea maji.” Akatawadha miguu yao, wajua, akiangalia. Kasema, “Karibu nina hakika niko sahihi.” Akamwendea Jamaa huyo mwingine, akamwangelia vizuri, wajua, na akatawadha miguu Yake, akapangusa mavumbi kutoka nguoni Mwake.

²²⁴ Akamwambia Sara, kasema, “Sasa, tayarisha mikate, upesi sana.” Na akawaambia watumishi, kasema, “Mchukueni huyo ndama ambaye ndiyo kwanza nimchinje.” Kasema, “Mkatakate. Na sasa tutawalisha Watu hawa.”

²²⁵ Akaendelea kuwatawadha. Kasema, “Sasa, nina hakika kabisa. Karibu nimejua yakini.” Na kwa hivyo basi baada ya kitambo kidogo . . .

Iliendelea, kwa kitambo kidogo. Wakaketi wakala.

²²⁶ Labda, walipokuwa tayari, baada ya kumaliza kula, waliendelea kuelekeza macho yao Sodom. Na baada ya kitambo kidogo, Mmoja wao akanena na kusema, “Ibrahimu.” Si Abram sasa. Siku chache tu hapo kabla, Mungu alikuwa amelibadilisha jina lake. “Ibrahimu, yu wapi Sara?” Si S-a-r-a-i; bali S-a-r-a, Sara. “Yu wapi mkeo, Sara?”

²²⁷ Alijuaje jina lake lilikuwa Ibrahimu. Alijuaje alikuwa ameo? Alijuaje alikuwa na mke. Alijuaje jina lake lilikuwa Sara? Alijuaje lilikuwa limebadilishwa kutoka Sarai likawa Sara, naye kutoka Abram akawa Ibrahimu?

²²⁸ Ibrahimu akasema, “Loo, jamani! A-ha! Huyu hana budi kuwa . . . Nilimwona katika Roho, bali huyu hana budi kuwa Ndiye.” Yeye. . . Ndipo Ibrahimu akasema, “Yuko hemani.” Nayo Biblia ilisema ya kwamba Mtu huyo alikuwa ameelekeza mgongo Wake hemani. Kasema, “Yumo hemani, nyuma, nyuma Yako hapo.”

²²⁹ Akasema, “Ibrahimu, nitakuzuru wakati uu huu mwakani. Umengojea kwa muda wa miaka ishirini na mitano sasa, kwa ajili ya jambo hili. Una umri wa miaka tisini sasa, ama umri wa miaka mia moja, naye ana tisini. Na sasa tutaninii . . .

Mimi, Mimi nitakuzuru sasa, na kuleta. Utampata mtoto huyu, niliyekuahidi. Loo! “Mimi” ni kiwakilishi nafsi. “Nilikuahidi.”

Ibrahimu akasema, “Ninajua ndivyo ilivyo sasa. Ninajua jambo hilo.”

²³⁰ Lakini Sara, huko nyuma chumbani, hakufahamu. Alisema, “A-ha!” Akachekeka, kasema, “Ati mimi, mwanamke mzee hapa, mwenye umri wa karibu miaka mia moja, na nipate raha pamoja na bwana wangu, na,” kasema, “Yeye akiwa ni mzee pia? Tungewezaje kuwa familia tena?” Kasema, “Tusingeweza kufanya jambo hilo.” Kasema, “Isingewezekana kamwe.” Naye akachekeka kimoyomoyo.

²³¹ Ndipo Mtu huyu, akiwa ameelekeza mgongo wake hemani, alisema, “Mbona Sara amecheka, akisema ya kwamba jambo hili lisingetendeka?”

²³² Ndipo Ibrahimu akajua. Ndipo Ibrahimu akajua. Ndipo Sara akajua. Naye akatokea, akitetemeka, kasema, “Sikusema hivyo kamwe.”

Kasema, “Naam, ulisema hivyo.”

²³³ Loo, ndipo Ibrahimu alishawishika ya kwamba ilikuwa ni Mungu. Akamwita, “Bwana,” herufi kubwa B-w-a-n-a, ambalo ni Elohimu. Si hadithi tu ya kujibunia; Yeye alikuwa Mungu. Yeye alikuwa ameketi pale. Kasema, “Loo!” Alikuwa ameshawishika kweli ya kwamba Huyu alikuwa ni Mungu.

Kwa hiyo, Yeye alikuwa akishuka kwenda Sodoma.

²³⁴ Naye alifanya nini? Ndipo alihusika kuhusu ndugu yake aliyepotea huko chini Sodoma. Upesi sana, alipoona yale yaliyokuwa yatendeka, akasema, “Nikiona watu hamsini kule chini ambao—ambao ni wenye haki, uta—utauokoa? Arobaini?” Na kuendelea chini kufikia, “Kumi.” Unaona? Alihusika juu ya ndugu yake.

²³⁵ Jambo ndilo hilo, ndugu. Tunahusika juu ya ndugu yetu wakati tunaposhawishika ya kwamba ni Mungu. Na kama sisi Wapentekoste tumeshawishika huyu ni Mungu, basi tutahusika kuhusu ndugu zetu. Hiyo ni kweli. Nasi tunatenda kana kwamba hatujashawishika kikamilifu. Na mara nyingi wakati tunapowaombea wagonjwa, ugonjwa unazidi tu kuendelea, unasema, “Vema, si—sijui. Niombee tena.” Tunaendelea, huku na huko, tunatenda kana kwamba hatujashawishika kabisa ya kwamba Mungu hutimiza ahadi yake.

²³⁶ Mungu hutimiza ahadi Yake, ndugu. Hakika, Yeye hutimiza. Kama si—si Mungu, kama si ahadi ya Mungu, basi haimbidi kuitimiza. Lakini kama ni ahadi Yake, Yeye hana budi kuitimiza, kusudi awe Mungu. Hakuna kitu kibaya na Mungu; iko kwa wewe na mimi.

²³⁷ Mungu aliahidi, katika siku za mwisho, yale angefanya, jinsi ambavyo angejidhihirisha katika siku za mwisho. Yesu alisema,

katika Yohana Mtakatifu 14:12, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.”

²³⁸ Wakati Filipo alipokuja pale, na mbele ya Yesu, naye akaona mambo haya yakitukia, alikimbia akampata Nathanaeli.

²³⁹ Nathanaeli akaja pale. Wakati Nathanaeli alipofika Mbele Zake, alishawishika kabisa, naam, bwana, wakati aliposema, “Nilikuona ulipokuwa chini ya mtini.”

²⁴⁰ Yeye alishawishika ya kwamba huyo alikuwa ni Masihi. Akasema, “Wewe ni Mwana wa Mungu. Ninajua.”

²⁴¹ Yule mwanamke kisimani, alishawishika kabisa wakati Yeye alipomwambia alikuwa na waume watano wakati huo. Alishawishika. Na hakushawishika tu, bali alihusika. Alikimbilia mjini na kusema, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyotenda. Yamkini huyu ndiye Masihi?” Unaona? Alishawishika kabisa, aliamini, alijua ya kwamba ilikuwa ni kweli.

Ee Mungu, uturehemu.

²⁴² Inatupasa kukaa pamoja Naye mpaka tumeshawishika, hiyo ni kweli, kujua kama ni kweli, ndipo tuone ahadi Yake imefanywa hai miongoni mwetu. Tungehusika. Kama tungechukua tu Kitabu cha Mungu hapa, na kusema, “Yeye aliahidi kufanya jambo hilo,” halafu tukae mpaka tumeshawishika ya kwamba Yeye ni Mungu wa Neno hili, kumwona Yeye akijidhihirisha katika Neno hilo, kulifanya Neno hilo hai, ya kwamba umepokea ahadi humu ndani. “Mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu. . .” Si moja tu la Hayo; Yote. “Na Maneno yangu yakae ndani yenu, basi ombeni mtakalo, mtatimiziwa.” Hiyo ni kweli. Unaona? Halina budi. . .

²⁴³ Si leo tu; usiku wa leo na kesho, unalitilia shaka. Unalitupilia mbali kesho, na kusema, “Vema, ninawaambia. Si—sijui kama ni kweli ama si kweli. Huenda lilikuwa ni kwa ajili ya mtu fulani; sijui kuhusu mimi.” Basi, unaona, halikai. Linaondoka. Unaona? Ndege wanapitia hapo na kuliokota, ndege wa angani.

²⁴⁴ Lakini kama likianguka lipitie moja kwa moja juu ya hoja yoyote, mashaka yoyote, ama chochote kile, litazaa mia moja kwa mia. Kuhusika!

²⁴⁵ Inanikumbusha. Nina Maandiko kadhaa zaidi hapa ninayotaka kuyarejea, lakini nitasimama kwa dakika moja, kusema jambo hili. Niliona hivi majuzi, katuni ndogo gazetini. Ninataka kumalizia, katika kusema jambo hili. Hilo lilingusa. Na ilikuwa ni ka—katuni, katuni nzuri mno.

²⁴⁶ Kulikuwako na mvulana mdogo. Alikuwa amealia vizuri Jumapili asubuhi, tayari kwenda kwenye shule ya Jumapili. Maskini nywele zake ndogo zimechanwa, na kofia yake mkononi mwake. Alikuwa tayari amenawa uso wake. Naye

alikuwa amekula kiamshakinywa chake na kula kitu fulani, na kusugua meno yake, kisha akawa tayari kwenda kwenye shule ya Jumapili. Naye alikuwa amesimama kwenye mlango wa chumba cha kulala cha baba na mama waliokuwa wamelala, akibisha mlango, akisema, “Ni nani kati yenu ninyi nyote atakayenipeleka kwenye shule ya Jumapili?” Kuhusika. Jambo ndilo hilo. Jambo tu ndilo hilo, marafiki. Kuhusika.

²⁴⁷ Je! mnatambua ya kwamba wajibu wa jiji hili la Tempe hapa, ninaamini, uko juu ya mabega yenu? Ninaamini ya kwamba Mungu amewafanya minara ya taa, kila mmoja wenu. Ninyi, ninyi mna wajibu wa dhambi za jiji hili, uko juu ya wahudumu, juu ya watu wa kanisa, wasafiri, tunaposafiri kupitia hapa. Hivi hamuamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema.

²⁴⁸ Nini? Hamwogopi. Hakika hamwogopi kumchukua Mungu kwa Neno Lake. Mungu hutimiza Neno Lake. Mungu si Mungu wa kusema ya kwamba Yeye ni kitu kimoja, halafu kingine. Unaona? Kama—kama Yeye akiahidi lolote, atafanya jambo hilo. Mungu hutimiza Neno Lake. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

²⁴⁹ Hivi hamwamini ya kwamba Yesu yule yule aliyefufuka kutoka kaburini, amerudi katika umbo la Roho Mtakatifu Naye yumo ndani yetu sasa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] “Bado kitambo kidogo na ulimwengu haunioni tena, bali ninyi mtaniona. Mtaniona, unaona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, unaona, hata ukamilifu wa dahari. Hata ukamilifu wa dahari, nitakuwa moja kwa moja pamoja nanyi. Sitawaacha wala kuwapungukia. Loo, niko pamoja nanyi daima, hata ukamilifu wa dahari. Unaona? Ulimwengu hautaliona, bali ninyi mtaliona.” Ulimwengu hauliamini. Ninyi ndinyi mnaoliamini. Hilo. . . Wale wanaoamini jambo hilo ndio wanaolipokea. Hiyo ni kweli.

²⁵⁰ Loo, sasa, marafiki, hii hapa siri. Hili hapa jambo ninalowataka mjue.

²⁵¹ Ni—nina furaha sana kuja kuzungumza nanyi usiku wa leo. Ninyi ni wasikilizaji wazuri sana. Nina furaha sana kuwa katika kanisa la Ndugu Groomer hapa. Ninaona, ninaamini ulikuwa mweka hazina wakati mmoja, ama kitu kama hicho, katika mmoja wa mikutano yetu, ama kitu kama hicho, ukimshughulikia katibu, mweka hazina, na kadhalika. Da—daima nilitaka kuja kwenye kanisa lake dogo. Aliniuliza, nyakati hi—hizo, “Ndugu Branham, njoo ukatuhutubie.”

²⁵² Kuna kundi lingine la watu ambalo ningetaka kulifikia, hilo ni hawa Wahindi hapa juu, juu kidogo tu ya mahali hapa, Wahindi wa—wa Navajo ama Apache, hawa watu wa thamani. Ninaikumbuka mikutano hiyo kule juu, jinsi tulivyokuwa nayo. Na popote pale nilipo, ningali Ninaweza kuikumbuka mikutano

hii ya kupendeza karibu na hapa pamoja na hao watu. Nami nina...

253 Ujumbe ule ule niliohubiri hapo mwanzo, ningali nina jambo lilo hilo. Ningali ninasimama vile vile. Ni Mungu, ewe rafiki. Nimeshawishika kinaganaga ya kwamba njia hii ya Roho Mtakatifu ni Mungu. Sasa, hilo ni Kweli. Ninaliamini kwa moyo wangu wote, sasa. Na kama tuki...

254 Huna budi kushawishika. Kama hushawishiki, basi huhusiki.

255 Sasa, kama sikuhusika, ama kushawishika ya kwamba njia ya Roho Mtakatifu ilikuwa sahihi, ningali ningekuwa katika kanisa la Kibaptisti, maana hao ni kundi zuri la ndugu huko katika kanisa hilo la Kibaptisti. Naam, bwana. Hao ndugu wa Kimishenari ni ndugu wazuri, baadhi yao. Bali ningali ninawapenda.

256 Nami nimeshawishika kabisa, hata hivyo, ya kwamba, kanisa, wakati umewadia kwa kanisa kubatizwa na Roho Mtakatifu, huyo ni Kristo akiingia ndani yako, akijitambulisha kwa miujiza. Sasa, Wa—Wabaptisti wanaamini hilo pia, na makanisa karibu yote mbali na Katoliki.

257 Wakatoliki hula mkate mdogo wa ushirika, wajua, kwamba ni, “Mungu akiwa katika mkate huo mdogo mwembamba.” Usiku mmoja nitahubiri juu ya jambo hilo, wajua, *Upagani Dhidi Ya Ukristo*, Bwana akipenda, kwa hiyo, kuhusu “mkate huu mdogo mwembamba ukiwa Mungu.”

258 Kwa hiyo, sasa, ni—ninaamini ya kwamba Waprotestanti wote wanaamini, na ule uamsho mkuu wa kiinjilisti wa walio—waliozaliwa kwa Roho wa Mungu, ama walio na Mungu yeyote kwao. Wanajua Roho Mtakatifu huja. Lakini hawasemi ya kwamba “Yeye...” Wakati ajapo, ya kwamba, “Amebadilisha tabia yake,” wanaonekana hivyo. Unaona? Wanawazia, “Vema, Yeye huuvumilia tu ulimwengu, na watu wanaweza kwenda moja kwa moja wakiishi jinsi walivyoishi daima, unajua, kwenda tu kanisani na kujaribu kuwa jamaa mzuri, kufanya vizuri sana uwezavyo.” Hilo silo, ewe rafiki.

259 Roho Mtakatifu anapoingia ndani yako, Yeye hukufanya kiumbe kipya. Naam, bwana. Anakufanya kiumbe kipya. Naye anaingia ndani yako, nawe ni sanamu yake. Wewe, anaishi ndani yako, akitenda kazi, akitenda kazi apendavyo ndani yako.

260 Sasa, nilisoma Agano la Kale kwanza, nami nikaona kile Mungu alichokuwa katika Agano la Kale kupitia kwa hao manabii. Nilikuja kwenye Agano Jipya, na nikachukua Agano Jipya. Nilikuta kwamba, Mungu yule yule wa Agano la Kale pia alikuwa ndiye Mungu yeye yule wa Agano Jipya.

261 Ndipo nikachukua kutoka Agano Jipya, kurudi chini kwenye kuundwa kwa dhehebu la kanisa Katoliki la mwanzoni, ambalo

lilikuwa ni yapata miaka mia tatu, huko kwenye Baraza la Nikea wakati maaskofu walipochukua jina la Papa na kanisa la Kirumi, na ambalo lilichukua upande wa fundisho la sharti. Nalo kanisa Katoliki la Kiorthodoksi liliamini Biblia na kuendelea. Lakini kanisa la Kirumi lilichukua kwenye—kwenye upande wa fundisho la sharti, na wangali wanafanya hivyo siku hizi. Na kwa hiyo basi, mle ndani, walipoteza miujiza na ishara. Hilo liliendelea kwa mamia ya miaka mpaka kwenye yale matengenezo.

²⁶² Ndipo yale matengenezo yakatokea. Kulitokea Martin Luther na John Wesley, ninaamini, malaika wa nyakati za kanisa, tulipopitia kwenye wakati wa Filadelfia na—na wakati wa Thiatira.

²⁶³ Na sasa kule chini kwenye wakati wa kanisa la Laodikia. Na tamasha ya kuhuzunisha sana ya jambo hilo ni wakati huo wa kanisa la Laodikia, kwa sababu Kristo alitupwa nje ya kanisa Lake, naye alikuwa akibisha, akijaribu kurudi ndani. Hiyo ni kweli. Naam. Hiyo ni kweli. Kanisa tunaloingia, akijaribu kurudi baada ya kutupwa nje.

²⁶⁴ Loo, ndugu, dada, jinsi Yeye anavyotaka kuingia miongoni mwa kanisa Lake! Jinsi anavyotaka kutenda kazi miongoni mwao! Jinsi anavyotaka kujielezea kwa—kwa ulimwengu! Anaweza kufanya jambo hilo tu wakati akinitumia mimi na wewe.

²⁶⁵ Walijuaje ya kwamba huyo alikuwa ni Masihi? Yule mwanamke kisimani alijuaje huyo alikuwa ni Masihi? Wakati alipomwambia ya kwamba alikuwa na waume watano. Nathanaeli alisemaje, “Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai?” Kwa sababu Yeye alisema, “Nilikuona ulipokuwa chini ya mti.” Unaona? Hivyo ndivyo wanavyojua. Hiyo ilikuwa ni ishara ya Masihi. Hiyo ni kweli. Hebu mwulize tu mtu yeyote. Angalia kote katika Biblia. Hivyo ndivyo ilivyo, ile ishara ya Masihi. Sasa Yeye ni . . .

²⁶⁶ Nimepitia humu nchini mara nyingi. Wala mimi—mimi si Masihi. Mimi—mimi ni ndugu yenu.

²⁶⁷ Lakini kile ninachojaribu kusema, ya kwamba, Masihi, Kristo, Roho Mtakatifu yule yule aliyekuwa ndani ya Kristo, huyo ndiye aliyemfanya kuwa Masihi. *Kristo* maana yake ni “Aliyepakwa mafuta.” Yeye alikuwa mwili wa nyama uliotungwa mimba katika tumbo la uzazi la mwanamke.

²⁶⁸ Na baadhi yenu ninyi Wakatoliki wazuri mnajaribu kumfanya mungu mke. Je! mlitambua ya kwamba yeye hakuwa zaidi ya kiangulio ambacho Mungu alitumia? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] La hasha. Yeye si malkia wa Mbinguni. Yeye alikuwa ni mwanamke tu ambaye Mungu alimchagua, mwanamke huyo, kwa maana alikuwa msafi na bikira, na akamjilia kwa Roho Mtakatifu na kuumba mwili ndani yake,

kwa uumbaji Wake mwenyewe. Mwanamke hakuwa na mbegu ndani yake, hata kidogo, hata kidogo. La, hasha. Ilikuwa . . .

²⁶⁹ Hakuwa Myahudi wala Mmataifa. Yeye alikuwa Mungu. Aliumbwa katika tumbo la uzazi. Na mwili huo mtakatifu, msafi, pasipo kuwa na mbegu kutoka kwa mwanadamu yeyote hata kidogo, ulikuwa chombo kitakatifu kilichotakaswa ambacho Yehova aliishi ndani yake. Kwa hiyo, Yesu alisema, “Si Mimi nifanyaye kazi. Ni Baba Yangu anayeishi ndani Yangu. Ndiye anayefanya kazi.” Hiyo ni kweli. Yeye angeweza kunena na kutaja maneno, kwamba ilikuwa ni nini. “Si Mimi. Ni Baba Yangu anayeishi ndani Yangu.” Unaona? Na, Baba Yake, hiyo ndiyo sababu aliomba kwa Baba. Yeye alisema . . .

²⁷⁰ Mtu fulani aliniuliza, kasema, “Vema, basi, Yeye angewezaje kumwomba Baba kama Baba alikuwa ndani Yake?”

²⁷¹ Nikasema, “Wewe unaombaje kwa Baba kama Baba yumo ndani yako?” Unaona? Jambo ndilo hilo. Unamwomba Roho Mtakatifu. Kwa hiyo, hakika unamwomba. Unaona? “Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.” Yehova Mungu aliye mkuu aliishi ndani ya Kristo. Sisi, Yeye yumo ndani yetu kwa kipimo. Yeye bila kipimo, sasa. Lakini, kipimo hiki kilicho ndani Yake, Kanisa lote pamoja katika Mwili. Unaona?

²⁷² Sasa tunaona ya kwamba, Mungu yule yule aliyekuwa katika Agano la Kale alikuwa katika Agano Jipya. Kurudi nyuma hata kwenye lile Baraza la Nikea, Yeye alikuwa angali ndani ya kanisa. Na hapa tunamwona, katika siku za mwisho, Mungu yule yule, Roho Mtakatifu yule yule, ishara ile ile, maajabu yale yale, miujiza ile ile, sura ile ile, jambo lile lile.

²⁷³ Sikilizeni. Mnajua mimi hufanya kazi ya umishenari. Nimezunguka karibu ulimwengu mzima mara saba. Angalieni. Huko katika nchi ambako watu hata hawajui mkono wa kuume ni upi na wa kushoto ni upi, Wasingeweza kuzungumza hata neno moja la Kiingereza cha aina yoyote. Baadhi yao, hawana hata lahaja. Ha—hawana sentensi wala chochote kile. Wanafanya tu namna fulani ya kelele za kuchanjachanja kama ndege. Wengine wanafanya kelele za kuchanjachanja kama wanyama wanaowasikia misituni; kulia kama tumbili, kugugumiza, kufanya kila namna ya makelele. Kamwe hawajasikia kitu kama Yesu Kristo wala kitu kingine chochote. Lakini, ndugu, hebu Roho Mtakatifu awashukie, wanafanya jambo lile lile mnalofanya papa hapa. Hiyo ni kweli. Kweli. Wao wanafanya jambo lile lile mnalofanya papa hapa Tempe, hiyo ni kweli kabisa, bila kuwambia lolote juu ya jambo hilo. La, bwana. Jambo pekee, Roho Mtakatifu anafanya jambo hilo. Wanafanya jambo lile lile unalofanya. Ni Roho Mtakatifu, ndugu.

²⁷⁴ Yeye ni Mungu Ujerumani. Yeye ni Mungu Uswisi. Yeye ni Mungu Arizona. Yeye ni Mungu kila mahali. Yeye ni Mungu juu

ya dari. Yeye ni Mungu katika sela. Yeye ni Mungu kanisani. Yeye ni Mungu ndani yako. Amina. Naam, bwana. Ninamwamini. Kila Neno alilonena ni BWANA ASEMA HIVI. Ninaamini Biblia hii ni Kweli. Amina. Je! mnaliamini jinsi hiyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

²⁷⁵ Je! kulikuwa na watu wowote wagonjwa humu ndani wa kuombewa? Inueni mikono yenu. Jana usiku tulifanya mstari mdogo wa maombi. Vema. Sasa, sikuja kanisani wakati huu...Sikuja, mwajua, kusambaza kadi zetu za maombi, na—na kuwaleta watu hapa, na labda kuwapata watu sita ama saba, kumi, ama kitu kama hicho, na kuwa mnyonge sana karibu inawabidi kunibeba kunipeleka nje. Nimekuja tu, nikiomba, kuwawekea mikono wagonjwa, na mambo kama hayo, yakiendelea.

²⁷⁶ Kweli, linaweza kufanywa vinginevyo. Hilo ni juu ya watu, unaona, ama juu ya Mungu, hasa, lolote Mungu analotaka kufanya. Lakini Yeye ni Mungu, sijali ni wapi, mambo rahisi tu.

²⁷⁷ Ndugu Welch, wakati yule nyoka alipokuuma, hakukuwako na ono juu ya jambo hilo. Kulikuwako? Nilimwekea mikono tu. Hivyo tu. Maana, Yeye ni Mungu.

²⁷⁸ Usiku mmoja, ama moja ya viamshakinywa mahali fulani, ninataka kuwaambia, jambo fulani lilitukia majuma machache tu yaliyopita, tangu mama yangu alipotuacha. Na nikiomba, nikiingia mwituni, na kuvaa tu nguo za ndani zenye joto, kuingia pangoni katika nyakati za baridi kali, hali ya hewa kule ni sufuri, na kukaa kule nje siku baada ya siku, na usiku baada ya usiku, nikiishi mbele za Mungu, mpaka akashuka na kusema nami, naam, bwana, na kuwa na uhakika ilikuwa ni kweli. Haina budi kuwa ni kweli. Sina budi kuwa na hakika na yale ninayozungumzia, kwa maana nina watu wanaoniamini mimi. Na nina watu wanaoamini ya kwamba ninawaambia Kweli, ya kwamba Mungu alinituma, naye Mungu anawajibika kusimama nyuma ya Neno Lake na kulitetea. Naye atafanya hivyo. Naam, bwana. Kama akikutuma, Yeye atathibitisha ya kwamba alikutuma. Kweli kabisa. Amina. Ninaamini hivyo. Nanyi je? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Amina.

²⁷⁹ Na—najua Yeye yuko hapa sasa hivi. Amina. Na kitu fulani tu kinachobubujika kote juu yangu sasa hivi tu. Ni—ninajua ya kwamba tumeketi usiku wa leo katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Amina.

²⁸⁰ Nitabadilisha nia yangu. Sitabadilisha nia yangu, bali Mungu ameibadilisha kwa ajili yangu. Amina.

²⁸¹ Sioni mtu ninayemjua hapa ndani, isipokuwa iwe ni bibi huyu anayeketi papa hapa. Huyu bibi pale, ninaamini aliombewa jana usiku. Wote walio wagonjwa, inua mkono wako. Wote wasionijua mimi, na wanajua sijui lolote kuwahusu ninyi,

ninamaanisha, inua mkono wako. Vema, kila mahali tu, nadhani. Hiyo ni kweli. Kama Mungu, Mungu yuyo huyo . . . Amina.

²⁸² Hii hapa changamoto. Angalieni kule, watu msiowajua, hamjapata kuwaona. Kama wewe ni mgonjwa, Mungu anajua wewe ni mgonjwa. Kama umevunjika moyo, Yeye anajua umevunjika moyo. Kama ulitenda dhambi, Yeye anajua ulitenda dhambi. Nena kuhusu muujiza!

²⁸³ Sasa, ingechukua nguvu za Mwenyezi Mungu kushuka na kuja kuthibitisha ya kwamba Yeye ni Mungu yule yule ambaye amekuwa daima, na angali ni Mungu. Kama atafanya hivyo angalau mara tatu katika jengo hili sasa hivi, mara mbili ama tatu, kama—kama thibitisho. Si—sijui kama atafanya hivyo au la. Lakini mimi nina ninii tu . . .

²⁸⁴ Ninaona saa hiyo ikifikia saa tatu na nusu. Ninajua, mstari wa maombi ukiwa na watu wengi namna hiyo, ungefikia hapa kwenye kama saa tano na nusu. Na ninajua Ndugu Norman anaendesha gari huko chini mbali sana, maili mia moja na kitu mpaka Tucson; watu mbalimbali. Na kesho usiku, ningali nina ibada kumi ama kumi na mbili, labda kumi bado za kuhubiri. Ninaninii tu . . .

²⁸⁵ Ninaamini hilo sasa hivi, kama mtaamini hilo pamoja na mimi, kwamba tuko katika ulimwengu wa Roho. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hebu niulize, na kuwathibitishia, ya kwamba Mungu angali ni Mungu vivyo hivyo tu alivyo papa hapa katika jengo hili usiku wa leo, kama alivyokuwa wakati yeye, Ibrahimu, aliposema Naye kule chini katika huo mwili wa nyama.

Kumbukeni, mwili huo, sijui ulikuwa ni kitu gani.

²⁸⁶ Wao walisema, “Thiofani.” Wahudumu wanajaribu kusema ilikuwa ni thiofani. Lakini thiofani inakulaje nyama choma? La, bwana. Thiofani haili.

²⁸⁷ Yeye alikuwa mwanadamu katika mwili wa nyama, bali hata hivyo ilikuwa ni Mungu. Hiyo ilikuwa ni ishara ya nini? Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu na za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu,” kwamba Mungu angeshuka chini aingie katika mwili wa mwanadamu na kujitambulisha Mwenyewe, kama tu vile Yeye alivyofanya huko nyuma. Hiyo ilikuwa, kumbukeni, hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya mwisho iliyotolewa kabla ya moto kushuka na kuiangamiza Sodoma na Gomora.

²⁸⁸ Na ulimwengu huu leo, na taifa hili, na watu hawa, wamekuwa kama Sodoma mamboleo. Hiyo ni kweli. Naye alisema nini? “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa; kula, kunywa, kuoana.”

²⁸⁹ “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu.” Ni kitu gani kilitukia wakati Lutu, katika siku za Lutu? Ni jambo gani

lilitukia? Angalia. Malaika alishuka, ama Malaika katika mfano wa mwanadamu. Naye Mtu huyu, akiwa na ninii Yake. . . Bila kumjua Ibrahimu, alimwambia kuhusu hali zake, na kuhusu Sara, na yale yatakayotukia, na yote kuhusu jambo hilo. Na hapo wakakuta kwamba, basi, ya kwamba Ibrahimu alikuwa ameshawishika ya kwamba huyo alikuwa ni Mungu, naye akaanza kumtetea ndugu yake. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mungu aliahidi jambo hilo.

²⁹⁰ Haidhuru, haikubidi uwe kanisa kuu mno. Haikubidi kuwa na ma—maelfu kwenye uamsho kule. “Popote wawili watatu wamekusanyika, niko kati yao,” kama Mungu atathibitisha jambo hilo usiku wa leo, anaweza kuyatambua mawazo yako.

²⁹¹ Nayo Bi—Bi—Biblia ilisema, katika Waebrania mlango wa 4. Sikilizeni kwa makini. “Neno la Mungu ni kali kuliko upanga uwao wowote ukatao kuwili, ukipenya hata kwenye mafuta ya mfupa.” Hiyo ni kweli? “Na hata huyatambua mawazo ya nia.” Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

²⁹² Neno la Mungu ni kitu gani? “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu.” Kwa maisha Yake mema na mwili Wake uliotakaswa, Damu Yake safi isiyoghoshiwa, Yeye aliitoa bure kwa ajili yetu sisi wenye dhambi wachafu. Na kupitia huo, Mungu alichukua dhahibu Yake na kulitakasa Kanisa, apate kumtuma tena Roho Wake Mtakatifu kuendeleza kazi alizofanya Yesu. “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.” Je! mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

²⁹³ Je! mnaamini ya kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu aliyezaliwa na bikira? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Je! mnaamini ya kwamba Damu Yake—Yake takatifu haikuwa kwa njia ya mwanadamu? [“Amina.”] Kwamba tunajua ya kwamba chembechembe ya damu hutokana na jinsia ya mwanamume, na kwa njia hii Mungu Mwenyewe Ndiye aliyeumba Damu na kumtoa Mwana Kristo Yesu. Naye alikuwa Mwana wa Yehova Mungu. [“Amina.”] Mungu aliishi ndani Yake. Na ndipo wakati alipoutoa Uhai Wake, ukombozi mtini, na akamwosha mwenye dhambi atakayemwamini Yeye, na amemchukua Yeye, na upatanisho wa dhambi zetu umefanywa, na ametuosha kwa maji ya Neno na ametusafisha, na sasa tunatakasika. Si wema wetu, bali rehema Yake, kusudi Roho Mtakatifu aendeleze kazi kwa Kanisa, kote katika wakati, kutangaza “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Amina.

²⁹⁴ Hilo lilipitia katika mambo matatu basi, “jana, leo, na hata milele,” safu tatu za kanisa. Amina. Hebu Mungu awaite kutoka kwenye safu hizo zote tatu basi. Mtaamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

Na tuombe.

²⁹⁵ Baba wa Mbinguni, Wewe tu ndiwe unayeweza kufanya jambo hili, bali ili kwamba watu hawa wajue, Bwana, ya kwamba wakati umekaribia. Huenda tusiishi mpaka asubuhi. Hatujui juu ya jambo hilo. Bali hatuna budi kukutana Nawe. Tuna hakika ya jambo hilo. “Kwa kuwa mwanadamu hana budi kufa kwanza, na baada ya jambo hili hukumu.” Inatubidi kukutana na Mungu mahali fulani.

²⁹⁶ Na, Baba Mungu, nimefundisha usiku wa leo ya kwamba Wewe ungali ni Mungu yule yule. Nao watu, Bwana, ninatumaini ya kwamba utajifanya halisi sana, kwa njia hii, Baba.

²⁹⁷ Wao, wamesikia mahubiri. Tuna baadhi ya wahudumu walio bora sana, ninaamini, Baba, walioko ulimwenguni, wanaishi humu nchini, na ni watu watakatifu sana, walijitolea kwa huduma ya Mungu, katika makanisa haya mazuri kote humu, humu nchini. Ninaamini hilo. Wao ni ndugu zangu. Nami nilikuja, Bwana, miongoni mwao, kama mgeni siku moja, nao walinipokea. Nao wakanikaribisha, nao wa—wananipenda.

²⁹⁸ Na—na, hata hivyo, mara nyingi ambapo inanibidi kukemea na kusema mambo. Ninawaona mara nyingi wakiambatana na shirika fulani, madhehebu yakiwaondoa kwenye njia ya kweli, ndipo ninawakemea. Na hata hivyo wangali ni watamu vivyo hivyo, na wananipenda, ndipo ninajua ya kwamba wao ni watumishi Wako, Baba. Nao wanajua ya kwamba sifanya jambo hilo nipate kuwa mwenye chuki; Bwana, usingejishughulisha na mtu kama huyo. Sasa, Baba, kujua ya kwamba hiyo, njia ya kurudi, ni kupitia kwa utakatifu, na kupitia kwenye utakaso wa Roho, na kuwekwa wakfu kwa maisha. Jalia watu . . .

²⁹⁹ Huenda kukawa na wageni hapa usiku wa leo. Huenda kukawa na Wapresbiteri, Methodisti, Katoliki, kundi fu—fu—fulani pamoja nasi usiku wa leo. Huenda ikawa kuna wale wasioamini. Na basi, Baba, kuhubiri Neno tu, wana haki ya kuondoka, labda, na kusema, “Mchungaji wangu anafundisha vinginevyo. Kasisi wangu anasema vinginevyo.”

³⁰⁰ Lakini, Bwana, wanapojua jambo Hilo, Biblia, madhehebu yote yanajua ya kwamba Waebrania 13:8 ilisema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Sasa, Wewe, Bwana, ya kwamba . . .

³⁰¹ Maskini mwanamke mmoja aligusa vazi Lako siku moja, akipenya kwenye umati, Nawe ukageuka, ukasema, “Ni nani aliyenigusa?” Na kila mtu alikanusha jambo hilo. Lakini zile nguvu kuu za Mungu zilizokuwa ndani Yako, ule utimilifu wa Mungu, Wewe uliangalia kote kwenye wasikilizaji mpaka ukamwona maskini mwanamke huyo aliyekuwa akitokwa na damu. Na ulipomwambia habari zake, kutokwa kwake kwa damu kulikoma. Kukakoma.

³⁰² Wewe ni Mungu yule yule. Ninaomba, Mungu, usiku wa leo, ya kwamba utawatakaswa waaminio hawa hapa ndani walio wagonjwa. Angalau mmoja, ama mmoja kutoka kwenye kila

safu, ama zaidi, Bwana, kuingama, nyuma, huko nyuma, waliosimama nje, popote pale, ya kwamba mtu fulani ataona, bila tashwishi yoyote, ya kwamba, “Hii ni Kweli. Roho Mtakatifu ni wa kweli. Na Biblia ni ya kweli. Na Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Ninaomba baraka hizi katika Jina la Yesu Kristo, na kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

³⁰³ Sasa, kwa wasikilizaji hawa wanaongojea, ninataka muombe kwa muda kidogo tu, mioyoni mwenu, nami ninawataka mwangalie upande huu. Ninataka muamini kwa moyo wenu wote ya kwamba Mungu yumo humu jengoni. Sasa, Yeye yuko katika Roho. Sote tunajua hilo. “Mungu ni...” [Kusanyiko linasema, “Roho.”—Mh.] “Nao wamwabuduo Yeye imewapasa kumwabudu katika Roho na Kweli.” Sasa, Kweli ni nini? Kristo, Neno. Neno ni ile Kweli. Roho ni Roho Mtakatifu. Neno ni Kweli. Naye Roho Mtakatifu huchukua Neno la ahadi na kulitimiza. Unaona? “Mkikaa ndani Yangu, Maneno Yangu ndani yenu, ahadi yoyote Mle ndani ni yako basi. Unaona? Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu,” basi sio ninyi. Ni Neno la ahadi linalofanya hivyo. Unaona? Ninatumaini unaona, enyi watoto. Nawatakia la heri.

³⁰⁴ Moja ya siku hizi tutasikia hotuba yetu ya mwisho huku chini. Mnajua hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ndipo tutapanda juu.

³⁰⁵ Nawe hebu sema tu, “Baba, Mungu, Ndugu Branham hajui lolote kunihusu mimi.” Labda hata hunijui mimi. Lolote, haijalishi uko wapi, mahali fulani tu jengoni. Unaona? Sema tu, “Baba, Mungu, yeye hajui lolote kunihusu mimi, bali hebu aseme nami na kuniambia shida yangu ni gani, ama kitu kama hicho, nami nita—nitakuamini Wewe. Nitakuamini Wewe, maana Neno basi, ninajua, ni mwili; pamoja na yeye na mimi, pamoja, tukiwasiliana na Mungu, Roho Mtakatifu yuko hapa. Jalia afanye hivyo.”

³⁰⁶ Huyu bibi aliyeweka mikono yake juu ya paja lake, namna hiyo, aliangalia juu na kusema, “Naam,” papo hapo, wakati akiitikia kwa kichwa chake. Aliamini. Ulisema tu jambo lifaalo.

³⁰⁷ Kulikuwako na mwanamke wakati mmoja, mwanamke Msirofoinike. Alikuwa ni Mmataifa. Alimjia Bwana Yesu, na kusema, “Bwana, Ewe Mwana wa Daudi, umrehemu binti yangu.” Sasa, Yeye hakuwa Mwana wa Daudi hata kidogo kwake. Alikuwa Mmataifa, unaona, kwa hiyo Yeye aliendelea kana kwamba hakumwona. Naye akamfuatilia akilia.

³⁰⁸ Na hatimaye akageuka, kasema, “Si vema Kwangu kuchukua chakula cha watoto na kuwapa mbwa.”

³⁰⁹ Loo, hilo si lingewafanya baadhi yetu tunaojiita Wakristo kufoka sana, kwa kuitwa mbwa! Kamwe hakufoka. Alijua hiyo ilikuwa ni kweli.

310 Kasema, “Hiyo ni kweli, Bwana. Lakini watoto... Lakini mbwa hula makombo chini ya meza ya bwana wao.”

Akasema, “Kwa kusema hivi, kwa sababu ulisema hivyo.”

311 Shinikizo la damu ulilo nalo na ugonjwa wa moyo, kama utaamini kwa moyo wako wote, utakuacha. Utakukubali? Unaona? Hiyo ilikuwa ndiyo shida yako, sivyo? Ni kweli. Liamini tu!...?... Amini. Sijapata kumwona mwanamke huyo maishani mwangu. Hatufahamiani.

312 Hapa, hebu tuone mwingine. Moja kwa moja juu yake, maskini mwanamke mdogo aliyevaa nguo ya kijani kibichi. Kama Mungu hatamsaidia mwanamke huyo, itambidi akafanyiwe upasuaji kwa ajili ya kivimbe. Hiyo ni kweli. Inua mkono wako, bibi. Sijapata kumwona maishani mwangu, bali yeye ana uvimbe. Unyonge na huzuni ya moyo wake! Kama utaamini ya kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, atafanya upasuaji huo na kukuondolea, bila upasuaji wa mkono mtu wa kawaida, unaweza kupata ulichoomba.

313 Je! Mmeshawishika? Mnaamini? Mtu mwingine jengoni, omba, amini kwa moyo wako wote.

314 Huyu hapa maskini bibi fulani anayeketi papa hapa, akiomba. Amevaa jaketi lenye miraba myekundu. Yeye ni mgonjwa na ni mnyonge. Ndiyo kwanza apate nafuu kutokana na nimonia. Hiyo ni kweli. Je! Unaamini ya kwamba Yesu Kristo atakuponya, bibi? Kama unaamini, inua mkono wako juu sana, na kusema, “Ninakubali.”

315 Akiketi moja kwa moja kando yake, huyo mtu hapo anayeumwa na mgongo, unaamini ya kwamba Yeye atakuponya, bwana? Basi inua mkono wako, useme, “Ninalikubali.”

Je! unaamini? Je! Umeshawishika? Basi husika.

316 Huko nyuma kabisa kuelekea upande wa nyuma, maskini mwanamke mdogo mwenye mvi anayeketi huko nyuma amejifunga kitambaa kidogo shingoni mwake, ana yabisi kavu mikononi mwake. Amekuwa akiomba kwa muda mrefu huo upate kuponywa. Je! unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, bibi? Unayeketi moja kwa moja *pale*, moja kwa moja *hapa* chini. Unaamini, ya kwamba Mungu ataiponya hiyo yabisi kavu? Unaweza kupata ulichoomba, endapo utaamini.

317 Mtu anayeketi karibu nawe pale, akiwa na ugonjwa wa tezi kibofu, kama utaamini kwa moyo wako wote, unaweza kuponywa. Unaamini, bwana? Ulikuwa ukijaribu kumfanya aamini, wala usingeweza kumfanya alione. Lakini Mungu alikuponya tezi kibofu wakati alipopitia karibu naye. Sasa ulipokea uponyaji wako. Mungu akubariki. Imekwisha. Imeondoka.

318 Jambo ndilo hilo. A-ha. Mnaamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mmeshawishika? [“Amina.”] Basi hebu na

tuhusike. Ninyi wengine mmeshawishika? [“Amina.”] Ni wangapi wanaohusika hapa? [“Amina.”]

319 Je! kuna mwenye dhambi aliyepo? Unahusika juu ya kikomo chako? Kabla hatujawaombea wagonjwa. Je! Unahusika kuhusu kikomo chako? Kama unahusika kuhusu kikomo chako, mbona usije hapa na kumpokea Kristo, wakati ukiwa moja kwa moja Mbele Zake hapa jukwaani. Njoni hapa. Njoni tu hapa juu. Watu wowote ambao—ambao wanahusika na wanajua ya kwamba hawako sawa na Mungu, ninawaomba usiku wa leo mje papa hapa madhabahuni, na msimame hapa kwa ajili ya maombi. Ndani ama nje, haidhuru uko wapi, tembea uje hapa juu. Mungu akubariki, mama. Hivyo ndivyo mnavyopaswa kufanya. Je! Yupo mtu mwingine anayehusika kuhusu mahali unakoelekea? Kama huna hakika kwamba uko sawa, nawe unahusika, njoo.

320 Je! mmeshawishika ya kwamba ni Kristo? Je! mmeshawishika ya kwamba—ya kwamba mimi, mwanadamu, nisingeweza kufanya mambo hayo? Je! Mmeshawishika ya kwamba Mungu aliahidi kufanya jambo hili katika siku za mwisho? Hilo ni Neno la Mungu. Yeye alishawi... Je! mmeshawishika kwa jambo hilo?

321 Niliona jambo lingine likitukia wakati uo huo. Mungu asifiwe! Watakuja kujua. A-ha. Vema. Sasa, Mungu asifiwe! Hilo ni zuri sana. Amina. Kama mkininii... Loo!

322 Mmeshawishika, mmeshawishika? Kweli mnaamini kwa moyo wenu wote? [Kusanyiko linasema, “Amina.” Mh.] Mtu fulani hapa ambaye huna uhakika kama uko sawa na Mungu, ama huko, mbona usije ukasimame hapa kwa maombi kwa dakika moja tu? Panda moja kwa moja uje tu huku. Sasa kama unaninii... Ama, hujashawishika ya kwamba uko sawa kabisa?

323 Baadhi yenu wanawake ambao mngali mnadai Roho Mtakatifu, na mna nywele fupi, mnataka kuniambia, baada ya mahubiri haya yote, bado hamjashawishika wakati Biblia ilisema yale iliyosema kuhusu mwanamke akiwa na nywele fupi? En-he? Na mnavaa na kutenda... Baadhi yenu wanaume ambao mngali mnavuta sigara na kufanya maovu? Baadhi yenu wanawake mnaovaa nguo hizi, na Mungu alisema ni chukizo Kwake?

324 Mnasema, “Mwili hauleti tofauti yoyote.” Basi kwa nini Mungu aliufufua mwili wa Kristo? Ni kwa nini tunapaswa kuishi maisha matakatifu, kama haumaanishi kitu? Huo, kweli, utafufuka tena, ule ufufuo. Kweli.

325 Je! Mnaamini kwamba huyu ni Roho wa Mungu, basi anakuhukumu. Hiyo ni kweli. Na utahukumiwaje? “Mwenye hatia kwa yaliyo madogo sana ana hatia ya yote.” Unajua kufanya vyema zaidi.

326 Mtu fulani alisema, kama nilivyotoa tamshi hilo jana usiku. Mtu fulani aliniambia, “Ndugu Branham, kwa nini usiwaache

wanawake hao? Waache hao wanaume. Acha kufanya hivyo.” Kasema, “Wewe ni . . . Watu wanafikiri wewe ni nabii.”

Nikasema, “Mimi si nabii kamwe.”

³²⁷ Akasema, “Watu wanadai wewe kuwa hivyo, hata hivyo. Kwa nini usiwafundishe kupokea karama za kiroho?”

³²⁸ Nikasema, “Ninawezaje kuwafundisha aljebra wakati hata hawajui ABC zao? Hawana adabu ya kutosha kujiosha na kutenda kama Wakristo. Utawaambiaje mambo ya kiroho kuhusu mambo ya Kimbinguni?” Hiyo ni kweli.

³²⁹ Hebu kanisa la Kipentekoste lijinyoshe, lijiweke sawa na Mungu, nami nitawathibitishia ya kwamba Roho Mtakatifu ataingia ndani moja kwa moja. Mbona, hili, kanisa, litajaa sana nguvu za Roho Mtakatifu, hakuwezi kuweko na mshiriki mmoja atakayefanya dhambi hata moja. Roho Mtakatifu ataitaja mara moja, kama vile Anania na Safira. Kweli. Lakini hamwezi kufanya jambo hilo, wakati hata hamtafanya elimu yenu ya shule ya chekechea. La hashu.

³³⁰ Njoni moja kwa moja, kwenye madhabahu, kama vile wanawake hawa wamefanya. Aisee, mnataka kusema kuna wanawake wawili tu katika kundi hili? Kumbukeni, ni juu yenu, na liko mikononi mwenu, wala hamtaweza kulinawa.

³³¹ Na tuinamishe vichwa vyetu. Njoni huku mbele sasa, wakati tukimwamini Yeye sasa, tunapoomba.

³³² Unasimama kwa ajili ya wokovu, pia, mwanangu? Nakutakia la heri, mwanangu. Simama papo hapo.

³³³ Sasa, tunapoinamisha vichwa vyetu, wanamleta bibi mwingine ambaye labda hawezi kutembea, ama kitu fulani, akija kupokea wokovu wa nafsi yake. Sasa tutaacha . . . Hilo ni sawa, acha tu asimame papo hapo. Hiyo ni sawa, dada. Haikubidi kutembea, kufanya hivyo. Yeye atakuja moja kwa moja kitini mahali ulipo. Hebu tuninii . . . Yeye anataka tu kufanya . . .

³³⁴ Sasa, kama mwanamke, ambaye anatembea kwa shida, nao wanayumbayumba huku, ameshawishika ya kwamba jambo hilo ni kweli, naye yuko tayari kuja na kutubu kwa ajili ya maovu ambayo amefanya, nanyi wanawake je! ambao, na wanaume pia, ambao mnaweza kusimama kwa miguu yenu na kutembea vizuri? Litatokea katika ile Siku ya Hukumu.

³³⁵ Eti kwa sababu tu tumevikwa jina la Pentekoste, hilo halimaanishi chochote. Huna budi kuzaliwa mara ya pili. Unapozaliwa mara ya pili, unatembea katika Nuru ya Biblia. Unafanya yale Biblia ilisema. Amina.

Na tuombe sasa.

³³⁶ Baba wa Mbinguni, Uwepo Wako upo hapa, na, loo, jinsi unavyotufanya tuzungumze kwa ujasiri wakati Uwepo

Wako ukiwa hapa, kwa sababu tunajua ya kwamba si sisi tunaozungumza wakati huo. Ni Roho Mtakatifu. Na, Ee Baba, jinsi mara nyingi inavyoudhi kusikia sauti ya—yako mwenyewe ikisema mambo ambayo usingeweza kusema, hata kidogo. Lakini basi, mtu yeyote angeweza kutilia shaka kwamba ni Roho Mtakatifu, baada ya wao kumwona akitenda kazi alizotenda wakati alipokuwa hapa katika mwili wa Bwana Yesu, kisha akatuachia ahadi ya kwamba Yeye angefanya kazi zile zile kupitia kwetu, watumishi Wake?

³³⁷ Na sasa, Baba, tunashukuru kwa ajili Yake kwa maana alikuja kuuhukumu ulimwengu kwa ajili ya dhambi. Dhambi ni kutokuamini. Wale wanaosema ya kwamba haliwezi kutendeka, hata hivyo inathibitisha ya kwamba imetendeka. Na kwenye kumbukumbu ya sayansi leo, tunajua ya kwamba umejithibitisha Mwenyewe kuwa pamoja nasi, kwa thibitisho nyingi zisizokanushika.

³³⁸ Hawa hapa watu hawa wamesimama wakiyazunguka madhabahu usiku wa leo, baada ya kutoa wito huu na kuhubiri Ujumbe huu, wa kushawishika na kisha kuhusika. Wanatambua ya kwamba maisha yao yamekuwa vivi hivi, nao ha—hawajaweza kufanya mambo ambayo wa—walitaka kufanya. Nao wanatambua ya kwamba hakuna lawama iliyowekwa juu Yako, bali wanatambua lawama imewekwa juu yao wenyewe. Kwa hiyo wamekuja usiku wa leo, Bwana, kutubu kwamba wamekosea.

³³⁹ Baadhi ya maskini wanawake hawa waliokata nywele zao, wanaosimama hapa, kama walivyofanya jana usiku, wakijua ya kwamba hiyo ni kweli. Biblia ilisema jambo hilo. Ni jambo la aibu. “Haipendezi kwa mwanamke kuomba akiwa na nywele zake kama kifuniko, akiwa amekata kifuniko chake? Anaajibisha kichwa chake.” Jinsi ambayo hayo ni mafundisho ya Kikristo! Na yule mwalimu mkuu aliyetufundisha jambo hilo, Paulo, alisema katika Wagalatia 1:8, “Ijapokuwa Malaika kutoka Mbinguni aje, akihubiri jambo lingine lolote isipokuwa lile ambalo nimewafundisha tayari, na alaaniwe.” Tunajua ya kwamba ni Kweli.

³⁴⁰ Na, Baba, wahudumu hawa wa thamani wakikemea jambo hilo, saa baada ya saa, saa baada ya saa, kusanyiko lingali likiyumbayumba. Jinsi ambavyo mioyo yao inatamani sana kuona kunisa lao lote limejazwa na Roho Mtakatifu, na kama wanaume na wanawake wacha Mungu wanaoketi pale. Na Roho yuna nguvu sana, mahali hapo, hata kila dhambi kanisani itatajwa, maajabu makuu na ishara kuu zitatendeka kama ilivyokuwa katika siku za mwanzoni.

³⁴¹ Na, Baba, ndipo tutaenda mahali mahali, tukishuhudia pamoja na ndugu zetu. Nao wanaona Roho Mtakatifu akitenda kazi kupitia matendo mbalimbali, na kujua ya kwamba

ni Mungu, ndipo watakuwa wamehukumiwa. Na kasema, Bwana. “Dhambi za watu wengine huwatangulia; wengine zinawafuata.” Wanatubu zao usiku wa leo, Bwana, zipate kuwatangulia. Ninaomba ya kwamba Wewe uwasaidie, kila mmoja wao, Bwana. Na sasa katika kuiweka wakfu mioyo yao Kwako, wanakutolea mioyo yao, maisha yao, kwa ajili ya huduma. Wanaweza kufanya jambo gani zaidi, Bwana?

³⁴² Sasa jalia Roho Mtakatifu, Ambaye alileta kushawishika kwalo, kwa Neno Lake na kwa Uwepo Wake, kuthibitisha Neno Lake, kulifanya Kweli kabisa, na awape sehemu inayotakasa ambayo itawapa shauku ya moyo wao, kusudi wakutumikie Wewe. Tujalie, Bwana.

³⁴³ Nafsi moja ya thamani pale ilisema ya kwamba adui alikuwa . . . Alikuwa tu akijaribu kuokolewa na kuwa sawa, naye adui akaendelea kumfanya aseme maneno mabaya dhidi ya Mungu, ama wawazo mabaya dhidi Yake. Ninaomba, Baba, sasa kama mtumishi Wako.

³⁴⁴ Ninamkemea huyo ibilisi. Mtoke mwanamke huyo. Achana naye. Mungu wa Mbinguni na amjaze kwa Roho Mtakatifu. Na, Shetani, huwezi kumfunga tena. Mwache huru. Acha aende, katika Jina la Yesu Kristo.

³⁴⁵ Kanisa hili, Kanisa takatifu la Mungu, linaomba kwa moyo mmoja, ya kwamba ibilisi huyo kamwe hatamrudia tena. Na aende sasa katika amani ya Mungu, kwa Jina la Yesu Kristo. Tunaweka wakfu jambo hili Kwako, Baba, kwa ajili ya utukufu Wako. Amina.

³⁴⁶ Sasa, bila tashwishi yoyote mioyoni na niani mwenu, sasa kwa msingi tu kwamba Mungu alifanya ahadi, nanyi mmekuja kuyaweka wakfu maisha yenu, na mnaamini kwa moyo wenu wote, mnaosimama hapa madhabahuni usiku wa leo, mkimwambia Mungu ya kwamba mnasikitika kwa ajili ya yale mliyofanya, ya kwamba mtaishi maisha tofauti tangu sasa na kuendelea. Je! unaamini Mungu hujibu ombi lako, nawe utaweza kufanya hivyo? Mwinulie mkono wako, useme, “Ninakukubali, Bwana wangu.” Amina.

³⁴⁷ Mungu awabariki. Hilo ni zuri. Sasa mnaweza kwenda kwenye viti vyenu na kujua yote yamekwisha. Ninaamini hilo. Je! Mnaamini hilo, kila mmoja hapa ndani? [Wale waliokuja mbele wanasema, “Amina.”—Mh.]

³⁴⁸ Sasa, ni wangapi wenu huko nje mlio wagonjwa, na ambao hamkupata . . . ambao Roho Mtakatifu kamwe . . . Maana, nimeona wanne ama watano. Ni, tayari, kwa namna fulani umeniacha sasa, huo utambuzi. Lakini nilikuona, mtu fulani *hapa* nyuma, ama, na halafu huko nyuma, umesimama huko nyuma. Lakini sikumbuki kwamba ilikuwa ni nini. Ile Nuru ilikuwa juu yao. Niliona kilichotukia. Lakini Roho Mtakatifu

yuko hapa, enyi marafiki. Mnaamini jambo hilo kwa moyo wenu wote? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

349 Sasa, ni wangapi hapa walio na ubatizo wa Roho Mtakatifu? Inua mkono wako. Vema. Biblia ilisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Je! mtawekeana mikono? Hebu niwaombe, kutoka jukwaani hapa.

350 Kwa hiyo, ni saa nne sasa, saa nne kasoro dakika tano. Je! ibada ya pili imetangazwa? Ni wapi mngeninii... [Ndugu Branham anazungumza na mtu fulani jukwaani—Mh.]

351 [Dada fulani anasema, “Ndugu Branham?”—Mh.] Naam, mpenzi. [Huyo dada anazungumza na Ndugu Branham.] Hakika.

352 Katika Jina la Yesu, na aondoke aende akaponywe yabisi hii kavu, na kamwe isimsumbue tena. Amina.

353 Nakutakia la heri. Ninajua itakuacha, nawe utakuwa mwanamume mzuri, mwenye nguvu na afya.

354 Mwenyezi Mungu, sisi ni watoto Wako, kwa imani katika Kristo Yesu. Sisi ni washiriki wa mwili wa Kristo, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Sisi ni wageni hapa duniani, wasafiri, tukijua ya kwamba Mbinguni ndiko nyumbani kwetu, wala haya si makazi yetu hapa, kwa hiyo tunayatazamia mambo yaliyo huko Juu. Sasa, tunaamini ya kwamba sisi tuko katika ulimwengu wa Roho katika Kristo. Jalia nguvu za Mwenyezi Mungu zikae juu ya jengo hili, na ziingie katika kila moyo.

355 Shetani, tunakuapisha kwa Yesu Kristo, Mungu aliye hai, ya kwamba uwaache watu hawa. Watoke, ewe Shetani, na uwaondoke, wapate kuponywa katika Jina la Yesu Kristo.

(Yeye tu.)

356 Ni wangapi wanaamini jambo hili? Ni wangapi wameshawishika? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ni wangapi wamehusika? Inua mkono wako, useme, “Mimi nimeshawishika. Nimeshawishika ya kwamba hii ni Kweli. Ya kwamba, sasa nimeshawishika ya kwamba kwa mapigo Yake nimeponywa. Sasa nimeshawishika ya kwamba ubatizo wa Roho Mtakatifu ni wa kweli. Sasa nimeshawishika ya kwamba Yesu Kristo yuko miongoni mwetu.”

357 Yohana alisema nini? “Yupo Mtu anayesimama miongoni mwenu, Ambaye hamumjui.”

358 Itanibidi kubadilisha sehemu hiyo yake usiku wa leo, na kusema yupo Mtu anayesimama miongoni mwenu, Ambaye hamwoni. Huyo ni Roho Mtakatifu. Yeye Ndiye, amina, anayefanya kila ahadi kuwa kweli. Mnaamini jambo hilo kwa moyo wenu wote, nafsi yenu yote, akili zenu zote? Simameni kwa miguu yenu na mlikubali basi, kama uponyaji wenu, kama wokovu wenu, chochote mnachoweza kuwa.

³⁵⁹ Kumbukeni ibada ijayo, kesho usiku, iko kwenye kanisa la Ndugu Outlaw. Ndugu Outlaw, huko Phoenix, kesho usiku.

³⁶⁰ Hebu na tuinue mikono yetu sasa na tumwimbie Mungu wimbo huu. Sijui kama naweza kuanza ama siwezi.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza.

Sote pamoja.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

³⁶¹ Sasa, ninyi mnaokuja na kuzifuatilia ibada, kesho usiku iko kwenye kanisa la Ndugu Outlaw. Linaitwa Kanisa la Jina la Yesu, huko Phoenix. Kwenye. . . Unalo, naam, ndugu, naam. Ndugu Groomer hapa ataitangaza. Vema.

³⁶² Bwana awabariki, mpaka nitakapowaona kesho usiku. Mungu awe nanyi.



KUSHAWISHIKA KISHA KUHUSIKA SWA62-0118

(Convinced Then Concerned)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Alhamisi jioni, tarehe 18 Januari, 1962, katika Kanisa la Full Gospel huko Tempe, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2010 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org